**Kama** una dalili hizi, shida afya ya akili inakunyemelea

UKURASA 3



**Neema** yanukia ziara ya kimkakati ya Rais Samia India

UKURASA 4



**MAISHA YALIVYO**

Mimba nje ya ndoa, anywa sumu kisa mumewe kaoa tena

UK. 11


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Oktoba 8, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581457

www.ippmedia.com



SUPA JACKPOT

TZS. 1,159,574,731

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#



www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## MALEZI YA WATOTO

# Mch. Kimaro aonya makosa 6 ya wazazi



• **Ahadharisha** kinatengenezwa kizazi cha ovyo *Endelea Ukurasa 4*

## YALIYOMO

UKURASA WA 18

**SIMBACHAWENE AWAPA RUNGU MAOFISA TAKUKURU RUSHWA MIRADI MIKUBWA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene amewataka wahitimu wa mafunzo ya awali ...

## Wastaafu 1,000 wamwangukia Rais wapewe mabilioni Shirika la Posta

UKURASA 3

## BAA LA SARATANI



# Aliyekatwa matiti atoa angalizo kwa kinamama

UKURASA 2


MICHEZO SIMBA, YANGA ZAKIRI 'KAZI IPO' UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Aliyekatwa matiti kwa saratani awapa angalizo kinamama

Na Romana Mallya

UGONJWA wa saratani unazidi kutafuna maisha ya watu na wengine kuwasababishia ulemavu wa kudumu.

Takwimu rasmi za serikali zinaonesha saratani zinazoongoza ni ya mlango wa kizazi kwa wanawake, ikifuatiwa na saratani ya matiti na ile ya tezi dume.

Mama wa watoto wanne anayeishi Marekani, Aisha Ramadhani (pichani), anasimulia namna alivyopoteza matiti yake yote kutokana na kuugua saratani.

Aisha anayetimiza umri wa miaka 50 mwezi ujao, ikiwa takriban ni miaka 10 tangu alipogundulika kuwa na saratani iliyosababisha kupoteza matiti yake, anasimulia milima na mabonde aliyokutana nayo hadi kupona tatizo hilo.

Katika mazungumzoa maalum na mwandishi wa habari hizi kwa njia ya simu, Aisha anaeleza changamoto alizopitia hadi kumsukuma kuandika kitabu cha 'Beyond the Diagnosis; Finding Faith and Strength Amidst Breast Cancer.'

Anasimulia kuwa kitabu hicho kinahusiana na mapito aliyopitia baada ya kugundulika kuwa na saratani ya matiti mwezi Januari 2014, alipofanya uchunguzi kwa mara ya kwanza na kulazimika kufanya operesheni mwezi Machi, 2014, yaani miezi mitatu baadaye.

Ilikuaje? Aisha anaeleza aligundulika kuwa na saratani miezi tisa baada ya kufiwa na mama yake mzazi nchini Tanzania, wakati huo yeye akiwa na umri wa miaka 40.

"Nina watoto wanne na kipindi hicho (alipogundulika kuwa na saratani) mtoto wangu wa nne ambaye ni binti alikuwa ana mwaka na miezi.

"Niliamua kitu ambacho kitanifaa kwangu mimi na familia yangu. Kwa vile nilikuwa na watoto wadogo kipindi kile na nilikuwa ninaogopa sana huko mbele maisha yatakuaje, nikaamua bora nikatwe matiti yote," anasimulia.

Anasema operesheni ya kukatwa matiti ilifanyika kwa siku mbili kabla ya binti yake wa mwisho kutimiza miaka miwili.

"Ni kitu ambacho kilinitia uchungu sana, lakini ninamshukuru Mungu kwa yote. Nilipogundua nina ugonjwa huu, niliogopa sana, nilikuwa na wasiwasi, nikawa ninawaza watoto wangu na maisha yao yatakuaje," anasema.

Anaendelea kusimulia kuwa wanaougua ugonjwa huo, wengi wanapitia changamoto nyingi, lakini kwake kwa kuwa ilikuwa katika hatua ya awali ilikuwa rahisi kwa madaktari kuchukua hatua za matibabu yaliyohitajika ili kuhakikisha anakuwa salama.

"Nilitakiwa kunywa dawa kwa muda kama miaka mitano baada ya operesheni, lakini nikatumia dawa kwa muda wa mwaka halafu daktari bingwa wa saratani akasema kuwa sihitaji tena kuendelea nazo.

"Kwa kuwa zilikuwa hazinisaidii tena na nilikuwa nimeshakatwa matiti yote, ambao ni uamuzi niliochukua. Daktari akasema hakuna haja mimi kuendelea kunywa dawa," anasimulia.



Kuhusu kitabu chake, Aisha anasema angependa kiwasaidie wengine wanaopitia changamoto kama hiyo wa kuwa yeye kilichomsaidia ni imani kwa Mungu na kitendo cha kuamua na kusema anamwachia kila kitu na kuamini atamweka salama, atamkinga na kumwezesha.

"Tunapitia mengi na mazito, lakini tukiwa na amani na tunamwachia Mungu kila jambo letu, ninaamini na nina uhakika kuwa Mungu anatuvusha na atatusaidia. Tangu nilipogundulika nina saratani mwaka 2014, ifikapo mwezi Januari 2024, nitatimiza miaka 10.

"Kuangalia vyakula ninavyokula na kujitahidi kuwa na amani moyoni mwangu na kuishi vizuri na kuzingatia afya yangu kwa kwenda kliniki mara kwa mara kuangaliwa ili kuhakikisha nipo salama. Ninapenda sana wanawake wenzangu na mabinti huko Tanzania wawe makini na afya zao," anasema.

Mama huyo anasema anapenda kujiunga na watu tofauti kama wanawake au vikundi ili kutafuta njia za kuwasaidia wanaopitia changamoto kama zake au zaidi.

"Kama mtu atakuwa anahitaji msaada au kufahamishwa vitu gani vya kufanya au kufuatilia afya yake na hili tatizo, nipo tayari.

"Kama mtu anahitaji kuongea na mtu au amsikilizie au ampe maelekezo, ni kitu ambacho nimeamua kuanzisha biashara ya kusaidia wanawake wanaopitia tatizo hili.

"Ninafanya kazi ya kushauri au kuwaongoza vitu vya kufanya au wafuatilie vipimo gani na namna ya kuwa na msimamo wa namna gani kuondokana na changamoto hii," anasema.

Anabainisha kuwa alipogundua amepata ugonjwa huo aliogopa hasa alipoiangalia familia yake ambayo mtoto wake wa kwanza kipindi hicho alikuwa ndiyo anaanza chuo.

Anaeleza kuwa hakutaka watoto wake waambiwe au wajue kinachoendelea, hivyo alichofanya ni kushirikisha tatizo lake kwa baadhi ya ndugu wa karibu akiwamo mume wake na bibi yake.

"Tuliamua watoto (wetu) tusiwaambie, hata baadhi ya wanafamilia wengi hatukuwaambia kwa kuwa hatukutaka hii hali na maneno yarudi kwa watoto. Lakini ndugu kama wawili, watatu walijua akiwamo dada yangu, bibi yangu niliyekuwa ninaishi naye na rafiki yangu mmoja," anasimulia.

Anasema anashukuru katika kipindi chote, mume wake alikuwa bega kwa bega naye, akimsaidia na hivyo kujiona ugonjwa huo siyo wake peke yake.

"Tukapambana na alikuwa ananisaidia sana. Kwahiyo, ninamshukuru Mungu kwa kuwa nilikuwa na mtu (mume) ambaye alikuwa pamoja nami mpaka mwisho na alielewa changamoto, uoga niliokuwa ninapitia," anasema..

Mama huyo anatoa wito kwa Watanzania wawe wazi na afya zao, ili wapate matibabu mapema kwa kuwa ugonjwa huo unapogundulika mapema huwa rahisi kutibika.

"Wasiwe waoga na wafuatilie vipimo. Kwa upande wangu, ninatafuta njia ili nije Tanzania na wenzangu wachache tutoe huduma hospitalini. Kazi ninayofanya ni 'mammograms' nilikuwa kwenye hii kazi nilipopata taarifa za huu ugonjwa. Nimefanya kazi hii kwa muda karibu miaka 20, ni kazi ninayoipenda," anasema.

Anasema akiwa kazini hupata nafasi ya kusaidia wagonjwa wengi hasa mabinti ambao wamegundulika kuwa na saratani katika hatua ya awali na huwahudumia.

Kadhalika anasema hufanya shughuli ya utoaji ushauri wa masuala ya saratani ya matiti.

"Ugonjwa huu ulipogundulika nilikuwa Marekani. Mimi ni Mtanzania ninayeishi Marekani. Nimeishi huku tangu mtoto, mama yangu mzazi alikuwa anaishi Tanzania na nina ndugu Tanzania na nimekuwa nikija Tanzania mara kwa mara kuwatembelea," anasema.

Mwanamke huyo anashauri Watanzania wafuatilie afya zao na kwa wanawake na mabinti wawe wanajipapasa matiti yao mara kwa mara ili kubaini kama kuna vivimbe au wafanye vipimo walau mara moja kwa mwaka.

Anawakumbusha kuwa kwa kufanya hivyo itasaidia kugundua tatizo katika hatua za awali na kupata matibabu na kupona.

Katika uzinduzi wa Mwongozo wa Tiba ya Saratani Tanzania sambamba na tamko la Waziri Afya, Ummy Mwalimu wakati wa maadhimisho ya Siku ya Saratani Duniani mwaka huu, wananchi walihamasishwa kufanya uchunguzi wa awali wa kupima saratani ya matiti ili kujua hali zao.

Waziri Ummy alisema Tanzania inakadiriwa kuwa na wagonjwa wapya wa saratani 42,000 kila mwaka ambao ndiyo hufika katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Alisema taarifa za mwaka 2022/23 zinaonesha Taasisi ya Ocean Road ilihudumia wagonjwa wapya takribani 8,779 na asilimia 13 kati yao sawa na wagonjwa 1,141 walikuwa na saratani ya matiti.

Mwaka 2022, Waziri Ummy alitaja saratani zinazoongoza nchini ni ya mlango wa kizazi kwa wanawake, saratani ya matiti na saratani ya tezi dume huku maeneo yanayongoza kwa wagonjwa wengi ni mikoa ya Kanda ya Mashariki asilimia 61 na Kanda ya Kaskazini asilimia 17.3.

# Neema yanukia ziara ya kimkakati ya Samia India

Na Mwandishi Wetu

WAKATI ziara ya kitaifa ya Rais Samia Suluhu Hassan ikitarajiwa kuanza leo India, msafara huo umetajwa kufanyika kwa wakati mwafaka; nchi hizo mbili zikihitajiana kiuchumi, kijamii na kiteknolojia.

Ingawa biashara baina ya Tanzania na wafanyabiashara kutoka Bara Hindi ina historia ya karne nyingi zilizopita na uhusiano rasmi wa kiserikali ukiwa umedumu kwa zaidi ya miaka 50, ziara hiyo ina ladha tofauti.

India iko njiani kuzipiku Japan na Ujerumani na kuwa taifa la tatu kwa uchumi duniani nyuma ya Marekani na China na inahitaji malighafi zaidi kukuza uchumi wake zaidi.

Tanzania ni miongoni mwa nchi za Kiafrika zenye uchumi unaokua kutoka kuwa nchi masikini hadi ule wa kati na tajiri. Inahitaji mitaji, uwekezaji mkubwa na soko la kuuzia malighafi zake duniani.

India inahitaji malighafi na mazao kutoka Tanzania ili kulisha watu wake wanaokisiwa kufikia bilioni 1.3. Tanzania inahitaji kutumia mitaji kutoka kwa matajiri wa India na utaalamu wa teknolojia na biashara zaidi ili kukuza uchumi wake.

Vitu vichache katika ziara hii vinaonyesha namna ziara hii ya Rais Samia - ya kwanza kufanywa na Rais wa Tanzania nchini India katika muda wa miaka minane, itakavyokuwa tofauti na za miaka iliyopita.

Mosi ni taarifa ya Waziri wa Mambo ya Nje, January Makamba, kuwa ujumbe wa wafanyabiashara takribani 80 wa Tanzania utafuatana na Rais katika safari yake hiyo.

Wafanyabiashara hao wanatoka katika maeneo ambayo ama yanatafuta masoko zaidi au yanayohitaji mitaji zaidi na ushirikiano kutoka India ili yapige hatua.

Kwa mujibu wa January, serikali tayari imetenga eneo la ekari zaidi ya 1,000 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda kutoka India ili kukuza uwezo wa uzalishaji wa taifa hili na kuongeza ajira kwa Watanzania.

Eneo lingine ambalo limepewa umuhimu wa kipekee kwenye ziara hii ni suala la afya. India kwa sasa ni miongoni mwa mataifa yanayoongoza kwa uzalishaji wa dawa na matumizi ya teknolojia ya kisasa kwenye matibabu.

Rais Samia amewahi kuzungumza hadharani kwamba anaguswa sana na changamoto za kiafya zinazowakabili Watanzania na ziara hii inajibu mojawapo ya changamoto hizo.

Waziri January aliwaambia waandishi wa habari kuwa Rais Samia atatia saini makubaliano ya uwekezaji kwenye utoaji wa huduma za kupandikiza figo nchini.

Tatizo la figo ni miongoni mwa matatizo yanayoongezeka nchini, yakiathiri watu wengi. Matibabu yake ni gharama kubwa na wenye uhitaji wa huduma hiyo huonekana kama wana hukumu ya kifo.

Kwenye ziara hiyo ya kihistoria, Rais Samia anatarajiwa kukutana na kufanya mazungumzo ya faragha na baadaye mkutano na waandishi wa habari na Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi.

Pia atakutana na kuhudhuria dhifa ya kitaifa aliyoandaliwa na mwenyeji wake, Rais Droupadi Murmu wa India mnamo Oktoba 9 mwaka huu.

## HABARI KITAIFA




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (kulia) na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (katikati), wakimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Swahili Knits, Hussain Halai (kushoto), wakati wa maonyesho ya kimataifa ya TIMEXPO 2023, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wastaafu Shirika Posta na Simu wamwangukia Samia stahiki zao

**Na Enock Charles**

ZAIDI ya wastaafu 1000 wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu wamemwomba Rais Samia Suluhu kuingilia kati ili walipwe stahiki zao zinazotokana na akiba na hisa katika benki na majengo walizodai zinafikia Sh. bilioni tisa.

Katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana uliohudhuriwa na baadhi ya wastaafu hao , Mwenyekiti wa Umoja wa Wastaafu hao, David Hango, akiwakilisha wastaafu wenzake, alisema licha ya kuwasilisha madai yao kwa viongozi mbalimbali wa serikali, mpaka sasa hawajalipwa fedha zao huku baadhi yao wakiwa wameshafariki dunia bila kupata stahiki zao.

"Mnamo mwaka 2019 tulikwenda kwa Meneja wa Chama cha Kuweka na Kukopa (KK) na kumtaka alipe stahiki zetu, lakini cha ajabu alisema chama hakina fedha za kulipa mpaka kiuzwe kiwanja ambacho ni mali ya chama kilichoko Mabibo," alidai Hango.

Akifafanua madai yao, Hango alisema ipo michango ya kila mwezi waliyokuwa wanachanga wakati wa kipindi chao cha utumishi katika lililokuwa Shirika la Posta na Simu. Baadaye vilitenganishwa na kupatikana Shirika la Posta na Shirika la Simu na hivyo kuwapo akiba ya wanachama inayofikia Sh. bilioni 1.2.

Pia alidai zipo hisa katika Benki ya TCB zinazofikia Sh. bilioni tatu na hisa za majengo ya Posta zinazofikia Sh. bilioni tano.

Aliiomba serikali kupeleka wakaguzi wa hesabu ili kukagua mali za chama hicho, akidai kuna matumizi mabaya ya mali za chama hicho ikiwamo miradi na hisa za wanachama, jambo linalopelekea kushindikana kulipwa stahiki zao.

Meneja wa Chama cha Kuweka na Kukopa cha Posta na Simu, Esau Mwasilembo, akijibu madai hayo, alisema uwekezaji wa chama hicho ni wa muda mrefu, hivyo si rahisi kulipa mtu mmojammoja anapostaafu na hivyo ni lazima kuuza mali za chama hicho ili kuwalipa.

Alisema uuzaji wa mali hizo si la jambo la muda mfupi kutokana na ugumu wa upatikanaji wateja.

"Kuuza hizo rasilimali ndiyo imekuwa changamoto Tuna hekari tano ziko Mabibo, Tathmini inasema kiwanja kina thamani ya Sh. bilioni mbili, lakini hiyo Sh. bilioni mbili tumetafuta mteja hatujapata.

"Hivi ninavyokwambia imetoka zabuni tumewapelekea watu wote, ikiwamo Manispaa ya Kinondoni, Manispaa ya Ubungo, kwamba tunauza huu uwanja kwa anayeweza kununua.

"Kama wakilipa tuweze kupata hela ya kuwalipa nje ya kuuza hivi vitu, ni ngumu kupata fedha ya kuwalipa na uamuzi wa kununua hivyo viwanja ni ya wanachama wenyewe," alisema Mbwilo.

Alisema tatizo kubwa linalowakabili kwa sasa ni baadhi ya mali hizo kutokuzalisha, hivyo kutokuwa na fedha za moja kwa moja na badala yake chama kinamiliki mali za pamoja, hivyo kuwapo ugumu wa kuwalipa wastaafu hao.

# TCAA yasema Tanzania ina upungufu wa marubani 150

**Na Beatrice Shayo**

MAMLAKA YA Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) imetaja changamoto saba zinazoikabili sekta hiyo ikiwamo upungufu wa marubani 150, uchakavu wa mitambo ya kuongoza ndege na miundombinu duni ya kuhudumia usafiri huo nchini.

Hayo yalibainishwa wiki hii jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Hamza Johari alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya miaka 20 ya kuanzishwa kwa mamlaka hiyo Novemba 1 mwaka 2003.

Alisema sekta hiyo inakua kwa kasi, lakini ongezeko la wataalamu haliko kwenye kasi hiyo.

"Mtu anajipanga kununua ndege, sisi kama sekta inatubidi tukimbie kuhakikisha tunakuwa na wataalamu stahiki katika hilo eneo.

"Kwa bahati mbaya watu wanaopenda kusoma masomo ya sayansi siku hizi wamepungua na sekta hii ni ya kitaalamu tuna upungufu wa marubani, wahandisi lakini zaidi kwenye marubani," alisema Johari.

Alisema kwa sasa wana marubani 603 kulingana na mahitaji ya soko, ukuaji wa soko na ndege nyingi zinavyonunuliwa, jumla walitakiwa wawe na marubani 780, hivyo wana upungufu wa marubani 150 kuendana na ukuaji wa soko.

Alisema hatua wanazochukua ni pamoja na kuanzisha mfuko wa marubani unaochangia fedha wanaozitumia kuwasomesha.

Alisema wamekuwa wanawasomesha masomo ya urubani nje ya nchi na gharama zake ni kubwa, hivyo hawawezi kupeleka wanafunzi wengi. Mpaka sasa wamewasomesha wanafunzi 22.

"Mifumo ya redio tuliyokuwa nayo ilikuwa ni ya muda mrefu, tumekuwa tunapata mrejesho kutoka kwa wateja wetu ambao ni mashirika ya ndege na rubani kuwa mifumo hii ya sauti wakati mwingine kumekuwa na mwingiliano na haina ubora unaotakiwa," alisema Johari. Alisema baada ya kukamilisha mradi mkubwa wa rada, wakaona waende kwenye mfumo wa sauti waibadilishe na kuweka mipya ili sauti iwe na ubora na kumfikia mlengwa ikiwa na ubora.

Alisema wanaweka mifumo mipya ya kisasa ambayo itaboresha mawasiliano ya sauti kati ya rubani na mwongozaji ndege. Mradi huo umeanza na unaendelea, utakamilika Aprili mwakani na tayari serikali imetoa fedha zote.

Alisema changamoto ya miundombinu ipo kwenye viwanja vya ndege. Si viwanja vyote vinafikika wakati wote.

Alisema wanatekeleza vyema majukumu yao. Mwaka 2003 wakaguzi walikuwa 28, kwa sasa wanao 44 (35 wakiwa ni wanaume).

"Bado tunahitaji kuongeza idadi ya wakaguzi na kama tulivyosikia Rais Samia Suluhu Hassan anaendelea kununua ndege, juzi tumepokea ndege na zipo nyingine nne zinakuja.

"Maana yake ni lazima tunyumbulike na soko na ukuaji wa soko na kuhakikisha kuwa tunakuwa na wakaguzi wa kutosha wanaoendana na idadi ya ndege zilizopo sokoni," alisema.

"Mwaka huo wa 2003 tulikuwa na ndege 101, leo hii zipo ndege 206 katika daftari letu la ndege lakini kwa upande wa udhibiti uchumi kazi yetu kubwa ni kuhakikisha usafiri wa anga unaendelea kuwa endelevu," alisema Johari.

Johari alibainisha kuwa mwaka 2003 idadi ya abiria kwa mwaka ilikuwa 1,521,000 na kwa sasa wameongezeka na kufikia 5,723,000 kwa mwaka jana.

Alisema serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri wa anga nchini ikiwamo upanuzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Dodoma, Abed Aman Karume, Mwanza, Iringa, Mtwara, Bukoba na hatimaye kuongeza uwezo wa kukidhi mahitaji yanayokua ya abiria na mizigo.


**MNADA WA HADHARA / NOTISI SIKU 30**

Tujijenge Tanzania Financial Services Ltd, tunatangaza notisi ya siku Thelathini (30) tangu tarehe ya tangazo hili gazetini kwa mdaiwa – **Fredrick Stephen Baraka** wa Dar Es Salaam aliyekopa na kushindwa kulipa deni la mkopo wake kulingana na makubaliano ya masharti ya mkataba.

**Fredrick Stephen Baraka** unatakiwa kulipa deni lako lote ndani ya siku 30, na mara tu baada ya notisi hii kuisha bila kulipa mnada wa hadhara utaendeshwa na **GEMSUD Investment Ltd** kwa kuuza gari kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini:-

| Mdaiwa/ mdhamini | Aina ya Dhamana | Tarehe ya mnada - Mahali |
|---|---|---|
| Fredrick Stephen Baraka | T 864 DCE, PASSO Rangi ya Silver | 22/11/2023 Makumbusho Yard |

**Masharti ya Mnada**
Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kukagua na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: 0652113262 / 0718068335**



**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT DELEGATE COURT OF MOROGORO AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.100 OF 2023**

**IN the Matter of the late JOHN EDMUND LYMO**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY;-**

**1.ANJELINA JOHN LYMO**
**2.........................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above-named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 12/10/2023.
Dated at Morogoro this 06 th day of OCTOBER 2023.

MAHAKAMA YA WILAYA MOROGORO

Resident Magistrate
PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE DISTRICT COURT MOROGORO



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**
**SHAURI LA ARDHI NA. 26 YA 2022**
**ATTORNEY GENERAL NA WENZAKE 2..............................WADAI**
**DHIDI YA**
**MILAGA HAMKA NA WENZAKE 40..............................WADAIWA**

**KWA: HILIWI JILALA**
**PILI MWASHULI**
**NDELE MANDE**
**MAGANGA MOTTO**
**LUHENGE MOTTO**
**JITIMA NDUBILU**
**MADUKA MUNGO NG'WANABEMBE**
**KITINYA MATONANGE**
**NGASA MOTO**
**JUMA PELEPELE**
**MWANAKUNDI UDULA GELEGELE**
**POPOTE MLIPO – TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI**
Mnaamriwa na mahakama hii, kuhudhuria hapa mahakamani tarehe 10/10/2021 siku ya Jumanne saa 3:00 kamili asubuhi bila kukosa.
**ELEWANI KWAMBA,** mkikosa kufika siku hiyo, shauri litasikilizwa bila ninyi kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na mhuuri wa mahakama leo hii tarehe 26/09/2023

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA



**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**GIDEON JORAM LYMO**
anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 671 CAT.**
Aina ya **TVS,**
Chassis No.
**MD625AF74J1E05287.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**PHQ /DOD/DOD/4812/2023.**



**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOSHI DISTRICT REGISTRY**
**AT MOSHI**
**APPLICATION FOR EXECUTION NO.42 OF 2023**

**RAVJI INVESTMENT COMPANY LIMITED......... APPLICANT**
**VERSUS**
**KIBO CORRIDORS LIMITED..........................RESPONDENT**

**TO: KIBO CORRIDORS LIMITED**

**NOTICE FOR MENTION**
**TAKE NOTICE:** That the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on 26th OCTOBER, 2023 at 09:00 am before **Honourable O.H KINGWELE –DR**

**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Mwananchi newspaper.

You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTE THAT:** In default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this 4th day of **OCTOBER , 2023.**

Deputy Registrar
HIGH COURT OF TANZANIA
MOSHI




Naibu Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Utawala na Fedha, Prof. Emmanuel Munishi (kushoto), akizungumza wakati wa kilele cha wiki ya huduma kwa wateja chuoni hapo, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine ni Naibu Mkuu wa chuo (Taaluma, Utafiti na Ushauri), Dk. Nasib Mramba (katikati) na Mkuu wa chuo hicho, Prof. Edda Lwoga. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## MCHUNGAJI KIMARO:

# Aanika makosa sita ya wazazi katika malezi

**Na Romana Mallya**

MCHUNGAJI wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Kijitonyama, Dk. Eliona Kimaro, ametaja mambo sita ambayo wazazi na walezi wanakosea katika malezi ya watoto.

Amesema mambo hayo yanachangia changamoto kwa taifa lijalo kutokuwa na uwezo wa kujitambua, kufikiri na kukosa kuelewa mambo.

Akihubiri katika maadhimisho ya Sikukuu ya Mikaeli na Watoto iliyofanyika Jumapili iliyopita, Mch. Dk. Kimaro aliwakumbusha wazazi wajibu wao katika malezi bora kwa watoto.

Mchungaji Kimaro alisema hakuna haja kuwanyima watoto kiboko pale inapostahili kwa kuwa wazazi ambao walikuwa watoto huko nyuma, nao walilelewa na viboko walipokosea, akiitaja ndiyo siri ya kufanya kwao vizuri hivi sasa.

"Mahubiri kama haya huwa ninatamani kukaa na bakora hapa, maana mnanikasirisha. Msizuie bakora, wamesoma wenyewe hapa wakati wanasoma mistari ya moyo.

"Wengine wananiletea watoto waombewe, kama ana tabia zinazohitaji bakora, ukiniachia mtoto, uende mbali, fimbo ni muhimu," alisisitiza.

Mch. Dk. Kimaro alibainisha kuwa mzazi mwingine anatoa sadaka ili mtoto wake apende kusoma na kuandika. Alisema mzazi wa aina hiyo hataondoa tabia hiyo kwa kutoa sadaka, bali fimbo.

"Mzazi mwingine anakuambia, 'usimpige mtoto, piga ngoma' mtoto atapigwa, hatuwezi kwenda hivyo, hizo haki za binadamu zinazozuia neno la Mungu, hiyo ni haki ya binadamu ya wapi inayokwenda kinyume cha neno la Mungu?" alihoji.

Alisimulia kuna mtoto wake ambaye alimwambia kuwa shule aliyompeleka ni nzuri, lakini kuna bakora.

"Aliponiambia hivi nikasema 'asante Yesu, kesho ninakwenda kutoa shukrani kanisani'. Nikamwambia mwalimu 'ukimpiga fimbo mbili, niongezee zangu ziwe sita'.

**SHIDA YA SIMU**

Mchungaji huyo alitaja jambo lingine ni wazazi na walezi kuwapa watoto simu au kompyuta mpakato kwenda nazo mahali pa kuabudu.

"Wazazi kwa bahati mbaya kuna mambo hayajakaa sawa, watoto wanapoletwa kanisani msiwape Iphone, simu janja, kishkwambi, kaa navyo kwenye gari. Watoto hawawezi kuja kanisani kuja kuangalia katuni, waangalie nyumbani, si kanisani," alionya.

Pia alisema tabia za watu zisizuie watoto kutambua kusudi lao la kuzaliwa, kujijua wao ni wavulana au wasichana.

"Nilikwenda nchi fulani nikamkuta mvulana wa darasa la sita. Nikamfurahia sana kijana alikuwa amevaa nguo vizuri na alifanya sala vizuri kwenye nyumba tulimokuwa tumekaribishwa.

"Nikamponngeza, lakini nilipotaja neno 'boy' (mvulana), wazazi wa nyumba ile wakaniambia 'usiseme mvulana mpaka atakapofikisha miaka 18, atachagua kama ni mvulana au msichana. (Wazazi) msiwazue watoto kujijua.

"Wakati tunakua, mama wakati mwingine alikuwa anatuambia 'wewe mwanamume gani?' Wewe utakuja kuwa baba wa namna gani? Waache wajue huyu ni baba wa kesho na huyu ni mama wa kesho, msiwazuie.

"Hili ninaliomba sana wazazi tulikazie sana, ukiwa na mtoto wa kiume mwonyeshe wajibu wake kama mtoto wa kiume tangu mtoto na ukiwa na mtoto wa kike mwonyeshe wajibu wake kama mtoto wa kike," alihimiza.

Mchungaji Kimaro alisema kuna ulemavu mkubwa kwenye akili za watu na walio wengi hawana mambo mapya kwa sababu ya uwezo mdogo wa kufikiri.

Alimpongeza Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda na jopo lake kwa kuja na maboresho ya mitaala ya elimu, akiamini sasa Tanzania itakuwa na elimu ya kufikiri kuanzia ngazi ya chini hadi elimu ya juu.

"Niliitwa kwenye kongamano moja, tulikuwa tunajadili kutoka mfumo wa kukariri hadi kufikiri. Dunia haihitaji watu wanaokariri, bali wanaofikiri, maisha hayatatengenezwa na watu wanaokariri, bali wanaofikiri, matatizo katika jamii yetu hayawezi kuondolewa katika jamii kwa watu wanaokariri, bali wanaofikiri kutatua matatizo," alisema.

"Ni hatari kulea mtoto kila kitu anakipata.

Sisi wakati tunalelewa miaka yetu, ukitoka shuleni unapita jikoni, unashika mafiga unakuta ya baridi. Tulikuwa tunakula limau tunaliona ni tamu, embe tulikuwa tunanyonya kwa kupokezana.

"Tulitembea kilometa 25 kwenda shuleni na kurudi nyumbani 25. Ninakwenda kubeba maji kilometa 15 na ndoo imetoboka, unachukua udongo au jani la mgomba unaweka yatakayofika nyumbani ndiyo yamefika na leo ndiyo mhubiri.

"Akili yangu siyo ya kuku wa kisasa, usijaribu watoto wako kila kitu, soda ya mgeni sawa, chakula sawa.

Hata Mungu hakumpa kila kitu Yesu, Yesu mwenyewe aliomba 'kikombe kiniepuke', lakini Mungu akasema no (hapana), kikombe hakikumwepuka, alisema ninaona kiu, hakumpa maji.

"Mtoto wako unamlelea akitoka kwenye school van (gari la shule) mtoto begi kule, soksi moja kule, dada wa kazi ndiyo akusanye," alionya.

# Kama una dalili hizi, shida afya ya akili inakunyemelea

**Na Romana Mallya**

WATAALAMU wamebainisha dalili ambazo mtu akiziona zinamtokea kwa kujirudia, atambue ananyemelewa na tatizo la afya ya akili.

Katika kilele cha bonanza la afya la waajiri lililoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE)wilayani Kinondoni, Dar es Salaam jana, watanzania, wakiwamo waajiri na wafanyakazi, walikumbushwa kuzingatia afya zao.

Mtaalam wa Saikolojia, Dk. Chris Mauki alisema watu wengi wamekuwa wakitafsiri afya ya akili tofauti na kuona watu wengine wakipoteza maisha bila kujua changamoto wanayopitia na namna ya kuwasaidia.

"Tukisikia tu afya ya akili, sura ya Milembe inakuja akilini, sura ya ukichaa inakuja kwenye akili yako na kujiona wewe ni mzima. Mwezi Oktoba 2022, utafiti ndani ya nchi ulionesha kati ya watu wanne Tanzania, mmoja ana changamoto ya afya ya akili," alikumbusha.

Vilevile, alisema zile nyakati mtu anajiona hayuko sawa na haumwi chochote, maana yake ananyemelewa na changamoto ya afya ya akili.

"Utajuaje? Kama ukiona mchakato wako wa kufanya uamuzi ni mgumu, unawaza kufanya uamuzi tofauti na ilivyo kawaida jambo ambalo ulikuwa unaweza kuliamua kwa dakika 10, sasa hivi unatumia siku tatu kuliamua, unanyemelewa na changamoto za afya ya akili.

"Kama ukiona unashindwa kulala vizuri, unakosa usingizi vizuri mpaka unywe pombe, fahamu kuna changamoto ya afya ya akili," alisema.

Dk. Mauki alisema kama mtu akiona anakwenda kitandani mapema halafu baada ya saa chache usingizi unakata, basi afahamu ana changamoto hiyo.

"Kama ukiona una ongezeko wa ghafla la uzito hususan wanawake wakati vyakula vyako havijabadilika, fahamu kuna changamoto ya afya ya akili kwa sababu baiolojia inaniambia changamoto ya afya ya akili inavyomvamia mwanamke, mfumo wa mmeng'enyo unakuwa chini," alisema.

Dk. Mauki alisema kwa mwanamume akiona anapoteza uwezo wa tendo la ndoa ghafla wakati hakuzoea hiyo hali, maana yake ananyemelewa na tatizo hilo, vivyo hivyo kwa mwanamke kupoteza hamu hiyo.

"Ukiona una hasira za mara kwa mara, unanyemelewa na magonjwa kama ya vidonda vya tumbo mara kwa mara, mshtuko wa tumbo, matatizo ya ngozi, ini, moyo... fahamu changamoto ya afya ya akili imekunyemelea," alifafanua.

Mtaalamu huyo pia alisema uhusiano mbovu ndani ya ofisi, ndoa na maeneo mengine umeonekana kuwa sehemu kubwa yanayochangia watu kupata shida hiyo kwa kuwa moyo wa binadamu asilimia 60 umetekwa na uhusiano.

Kuepukana na changamoto hizo, mtaalamu huyo alisema kuwa kwa walioko kazini, waajiri waweke mipango ya kusaidia wafanyakazi kwenye mipango yao ya afya ya akili.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Sadi Mtambule, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alisema katika miezi minne wilayani mwake, miongoni mwa mambo yanayosumbua ni afya ya akili kwa wananchi.

"Miezi miwili iliyopita tuna vifo vya watu sita, hivi vya kujinyonga. Mfano mzuri ni hapa Kijitonyama ambako mwezi Juni mwaka huu, mtu alijirusha ghorofani. Matukio mengine yalitokea Mikocheni na Mbezi, mtu anaamua kutoa maisha yake kwa sababu ndogondogo tu," alisema.

Katibu Mtendaji wa ATE, Suzanne Ndomba-Doran, alisema maadhimisho hayo mwaka huu yamelenga kuhamasisha umuhimu wa kuimarisha afya ya akili mahala pa kazi.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Herry Mkunda, aliipongeza ATE kwa kuja na mjadala huo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, aliyemwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema umuhimu wa bonanza ni kuimarisha afya ambao ni mtaji kwa wafanyakazi na waajiri.

Alisema bila ya kuwa na wafanyakazi wenye afya njema, hawawezi kuwa na uzalishaji wala kufanya biashara kama taifa.

HABARI KITAIFA

# Waziri Silaa abana maofisa ardhi

**Na Munir Shemweta,**
ARUSHA

WAZIRI wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa amewaelekeza wataalamu wa sekta ya ardhi nchini kuhakikisha mipango yote ya kupima viwanja inaendane na miundombinu ya maeneo husika.

Silaa alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na viongozi na watendaji wa sekta ya ardhi katika ziara yake ya kikazi ya siku moja mkoani Arudsha.

"Wataalamu wote wa sekta ya ardhi nchini mnapoandaa mipango ya upimaji viwanja mhakikishe ina miundombinu itakayosaidia wananchi wanaouziwa viwanja kupunguza gharama za makazi na maisha yao," alisema

Alisema ili sentesi ya jina la Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikamilike, lazima wataalamu wanapopima viwanja basi viwanja hivyo viwe na uwezo wa kusaidia huduma za miundombinu kwenye nyumba iliyojengwa pamoja na makazi.

Kwa mujibu wa Silaa, suala hilo lazima liendane na aina ya uendelezaji au ujenzi ili mhusika afahamu kama kiwanja alichochukua atajenga nyumba ya aina gani kama ni ya chini ama ghorofa.

Akielezea zaidi kuhusu zoezi la Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK) Silaa, alisema katika kipindi hiki anachohudumu wizara hiyo mkazo wake mkubwa utakuwa kwa zile K mbili za Kupanga na Kupima huku akisisitiza maeneo yote yanayoenda kupimwa ardhi basi wataalamu wasijifungue kama wataalamu wa fani moja na kuwaachia watu vichaka.

"Mipango sasa ya kupanga na kupima iende ikahusishe miundombinu ya barabara, maji, umeme, maji taka na mkongo wa mawasiliano ili mtu atakayekabidhiwa kiwanja awe anaweza kuishi.




Meneja wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Tawi la Same, mkoani Kilimanjaro, Mohamed Amri (wa tatu kushoto), akishirikiana na wateja wa benki hiyo juzi, kukata keki kusherehekea wiki ya huduma kwa wateja. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Kapinga ahamasisha matumizi nishati safi kutunza mazingira

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

NAIBU Waziri wa Nishati, Judith Kapinga amehamasisha wananchi kuona umuhimu wa kutumia nishati mbadala ili kutunza mazingira.

Akizungumza katika kikao cha Baraza Maalum la Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Ruvuma, alisema wananchi wakiwamo vijana wanafahamu mambo yanayoendelea duniani pamoja na mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema wizara yake kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA) imejipanga kwa kuwa na mikakati endelevu ya kuhakikisha wananchi wanaepukana na matumizi ya nishati ambayo siyo rafiki ya mazingira.

Kapinga ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum kupitia vijana, alisema serikali imejikita katika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi bora ya nishati safi.

"Rais (Samia Suluhu Hassan) kwa kutambua hilo kupitia wizara na REA tunaendelea kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ili kila mwananchi aweze kufahamu faida na hasara ya kutumia nishati ambayo si rafiki kwa mazingira," alisema.

Alisema matumizi ya nishati mbadala si kwa wanawake peke yao, bali hata wanaume wanapaswa kufahamu umuhimu wake.

Kapinga amewataka wajumbe wa Baraza la Vijana mkoani humo kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi kuanzia ngazi ya chini ili kusaidia kuondoa matumizi ya nishati ambazo siyo rafiki.

Mhandisi wa Mradi wa REA, Kervin Tarimo, akitoa elimu kuhusu matumizi bora ya nishati, alisema serikali imeweka mipango yakinifu inayohusiana na utunzaji wa mazingira.

Alisema wana mpango endelevu wa kutoa elimu ya umuhimu wa kutunza mazingira kwa wananchi kwa miaka mitatu ili kila mmoja aweze kuwa na uelewa.

Alisema sambamba na hilo, wametoa majiko banifu 70,000 yenye thamani ya Shilingi bilioni nne kwa baadhi ya wananchi mkoani humo.

Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Ruvuma, Kelvin Challe, alisema elimu hiyo italeta mafanikio makubwa kwa mkoani humo na nchi kwa ujumla.

## Zahanati Segerea, Kinyerezi, Kiwalani zapandishwa hadhi

**Na Pilly Kigome**

ZAHANATI tatu zilizipo katika Jimbo la Segerea, jijini Dar es Salaam zimepandishwa hadhi na kuwa vituo vya afya ili kutoa kipaumbele cha afya ya mama na mtoto, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan.

Zaidi ya Sh. milioni 300 zimetumika katika hatua za awali za kupandisha hadhi zahanati za Kinyerezi, Segerea na Kiwalani ili kuondoa changamoto na msongamano wa wananchi kupata huduma katika hospitali za rufani.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Dk. Zaituni Hamza, akizungumza na waandishi wa habari, alisema wamegawa vifaa tiba katika zahanati hizo ikiwa ni agizo alilolitoa Rais Samia katika kuzipandisha hadhi ili kuboresha huduma za afya.

Dk. Hamza alisema Rais Samia ameagiza kuboresha huduma za afya katika zahanati zote nchini ikiwa ni kukabiliana na afya ya mama na mtoto na kuondoa msongamano wa wagonjwa katika hospitali za Rufani za Amana, Mwananyamala na Temeke.

"Tunasubiri majengo yakamilike na zahanati hizi zitakwenda kuwa vituo vya afya, kwani wanawake watajifungulia, kufanyiwa upasuaji na kulaza wagonjwa wengine," alisema .

Mbunge wa Segerea (CCM), Bonnah Kamoli, amemshukuru Rais Samia kupitia Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu kwa kuwapatia vifaa tiba na kupandisha hadhi zahanati hizo kuwa vituo vya afya.

Alisema wananchi wa Segerea walikuwa wakikabiliwa na changamoto ya kukosa vituo vya afya na kujikuta wanakwenda umbali mrefu kufuata huduma za mama na mtoto na magonjwa mengine.

"Sina cha kusema zaidi ya kuwa na furaha kuona jimbo langu na wananchi wangu kuletewa huduma karibu. Ninamshukuru sana Rais Samia kwa kuthamini wananchi wa Segerea.

"Ni dhahiri kuwa tunatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwani, tuliwaahidi wananchi kuwaletea vituo vya afya kabla ya 2025," alisema.

Baadhi ya wananchi waliiambia Nipashe kuwa wanaanza kuiona Segerea mpya kwa kuwa wataepukana na adha ya kwenda umbali mrefu kufuata huduma za afya.

Katika Zahanati ya Kinyerezi wamekabidhi mashine moja ya usingizi, vitanda 25 vikiwamo 10 vya kujifungulia, shuka 200, mashine za kupima mapigo ya moyo 10 na baiskeli za wagonjwa mahututi.

Kwa upande wa zahanati za Segerea na Kiwalani zilikabidhiwa vitanda 25, shuka 500, viti vya wagonjwa 10, mashine za kupima mapigo ya moyo.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Upotevu wa maji udhibitiwe kuokoa mabilioni

**MAJI** ni muhimu kwa viumbe vyote duniani. Bila maji hakuna uhai. Maji ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Ili Watanzania wapate huduma ya maji, serikali kupitia Sheria Na.5 ya mwaka 2019 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, pamoja na mambo mengine, ilianzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA). Jukumu lake kuu ni usimamizi wa maji, usafi na mazingira vijijini.

Hata hivyo, licha ya kuwap RUWASA, bado kuna changamoto katika usimamizi wa rasilimali maji. Kwa kipindi cha miaka minne mfululizo, kuna upotevu wa maji yenye thamani ya Sh. bilioni 476.74, kwa mujibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Upotevu wa maji ni kipimo muhimu cha ufanisi na utendaji wa Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira nchini. Ni kipimo hicho kinachoangazia kutathmini ya kiasi cha maji kinachozalishwa au kununuliwa lakini hupotea kabla ya kufikia wateja.

Upotevu wa maji huwasilishwa kwa asilimia na hufanyiwa tathmini kwa kutoa kiasi cha maji kilichouzwa kwa watumiaji kutoka kwenye jumla ya kiasi kilichozalishwa au kununuliwa.

Kwa mujibu wa ripoti ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa mwaka 2021/22, sababu zinazochangia upotevu wa maji ni pamoja na uchakavu wa miundombinu ya zamani inayosababisha uvujaji maji na uunganishaji haramu unaopelekea kupotea kwa mapato.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeweka kiwango cha upotevu wa maji kinachokubalika kuwa kisizidi asilimia 20, lakini kwa kipindi cha miaka minne mfululizo, CAG amebaini kiwango cha upotevu wa maji kwa mamlaka 23 za Maji Safi na Usafi wa Mazingira kinachozidi kiwango cha asilimia 20 kinachokubalika.

Kwa mwaka 2021/22 upotevu wa maji ulikuwa jumla ya Sh. bilioni 162.14 tofauti na mwaka 2020/21 ambapo upotevu ulikuwa wa Sh. bilioni 175, hivyo kiwango cha upotevu wa maji kwa kipindi cha mwaka mmoja kimeshuka kwa Sh. bilioni 13.

Kupitia hotuba yake ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa Wizara ya Maji kwa mwaka 2022/23, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso anakiri upotevu wa maji nchini umeendelea kuwa changamoto kwa sekta ya maji na umeendelea kusababisha hasara kubwa kwa Mamlaka za Maji zinazotekeleza na kusimamia miradi ya maji nchini.

Waziri anabainisha kuwa mwaka 2021/22, hali ya upotevu wa maji nchini ilifikia asilimia 36.2, kiwango ambacho kipo juu ya kiwango kinachokubalika kimataifa cha asilimia 20. Hali hiyo kwa sehemu kubwa inasababishwa na uchakavu wa miundombinu ya kusambaza maji; hujuma katika miundombinu ya maji na wizi wa maji kwa kufanya maunganisho yasiyo ya halali kwa kutumia vishoka.

Nipashe Jumapili, tukiwa sehemu ya wadau wanaohimiza uwajibikaji, tunashauri changamoto hizo zitatuliwe ili kudhibiti upotevu wa maji, kwa kuziwezesha mamalaka za maji katika ukarabati na uboreshaji miundombinu chakavu ya maji.v

Vilevile, tunashauri elimu itolewe kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kulinda miundombinu ya maji pamoja na kurekebisha Sheria za Maji ili kutoa adhabu kali kwa wezi wa maji na wahujumu miundombinu ya maji.


Nipashe Jumapili pia tunaona kuna haja kufunga dira za maji zikiwamo dira za malipo ya kabla na kuanzisha mfumo wa pamoja wa ankara za maji ambao unasaidia kudhibiti upotevu wa maji kwa sababu unamtaka msomaji wa mita kufika na kusoma matumizi halisi ya maji katika mita husika.

Wakati hayo yanafanyiwa kazi, pia kuna haja mamlaka za maji chini ya usimamizi wa Wizara ya Maji, ziendelee kufanyia kazi sababu za kuongezeka upotevu wa maji ili kuepuka hasara.

Shime, upotevu wa maji udhibitiwe kuepuka hasara ya mabilioni ya shilingi na kuchochea uwajibikaji katika mamlaka za maji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tufanyie kazi angalizo la Waziri Ummy ulaji matunda mchanganyiko

Na Sabato Kasika

**MATUNDA** yanatajwa kama sehemu ya mimea yenye mbegu au yasiyo na mbegu ndani na ni sehemu ya chakula kinachojumuishwa katika lishe ya kila siku. Yana virutubisho vinavyohitajika mwilini.

Na ulaji matunda unategemea na jinsi mtu anavyopenda. Wapo wanaokula tunda lenyewe kama lilivyo au kuchanganya na matunda mengine, huitwa saladi ya matunda.

Faida kuu za matunda zinatajwa kuwa ni kuzuia maradhi, kurutubisha, kuongeza kinga ya mwili, kupunguza sukari kwenye damu, kung'arisha ngozi, kuongeza nguvu na kujenga mafuta asilia mwilini.

Kutokana na faida hizo, baadhi ya watu, hususani wakazi wa mijini, wamezoea kuchanganya matunda kwa mtindo wa saladi na kula, kitendo ambacho sasa kinaelezwa kuwa ni hatari kiafya.

Miongoni mwa matunda ambayo huchanganywa pamoja ni vipande vya ndizi, papai, embe, nanasi, parachichi na tikiti maji. Ni kawaida kuwakuta watu wa mjini wanakula.

Wengine wanauziwa ofisini, mitaani na hata wenye mtindo huo majumbani mwao, lakini Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu anasema mtindo huo wa kula matunda mchanganyiko una madhara ya kiafya.

Kutokana na hali hiyo, waziri huyo ametoa onyo alipozungumzia ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza ifikapo 2030 na kufafanua kuwa mtindo mbaya wa maisha ikiwamo ulaji usiofaa ni chanzo cha magonjwa hayo.

Ni angalizo alilolitoa wiki hii wakati wa uzinduzi wa kampeni ya uelimishaji kuhusu magonjwa yasiyoambukiza ulioambatana na uzinduzi wa mwangozo wa mtindo wa maisha na magonjwa yasiyoambukiza.

Katika ufafanuzi wake, waziri huyo anasema ulaji matunda mchanganyiko ni hatari kwa ugonjwa wa kisukari, huku akiitaka jamii kuacha kuchanganya matunda wakati wa ulaji.

> **Ni angalizo alilolitoa wiki hii wakati wa uzinduzi wa kampeni ya uelimishaji kuhusu magonjwa yasiyoambukiza ulioambatana na uzinduzi wa mwangozo wa mtindo wa maisha na magonjwa yasiyoambukiza.**

Waziri anasema kwa sasa nchi inashuhudia ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza hususan shinikizo la juu la damu, kisukari, saratani na mengine kutokana na mtindo wa kula mchanganyiko wa matunda.

Kwa onyo hilo la waziri, ninadhani ni vyema kushirikiana na wadau wa afya kuhamasisha jamii kuachana na mtindo huo, ili kusaidia watu kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu njia sahihi ya ulaji matunda.

Angalizo hilo la Waziri Ummy linaibua hoja ya umuhimu wa jamii kuzingatia ulaji ili kuepuka kukumbwa na magonjwa.

Ni kweli ulaji wa matunda kwa wingi unasaidia mwili kupata faida zikiwamo za kupunguza hatari ya kupata magonjwa ya moyo na kiharusi na kinga ya mwili dhidi ya aina za saratani, lakini yaliwe kwa mpangilio sahihi ili kuepuka madhara.

Wataalamu wa afya wanatolea mfano baadhi ya matunda kama maembe kwamba yanasaidia kulinda mwili dhidi ya magojwa kama shambulio la moyo na kisukari kutokana na kuwa na nyuzi.

Lakini pia wanaeleza kuwa yanasaidia kupunguza madhara ya uvimbe unaotokana na kuwa na chumvi nyingi mwilini. Kinachotakiwa ni kula tunda moja na siyo kutengeneza mchanganyiko wa matunda.

Vilevile, matunda yenye potasiamu kama ndizi kwa wingi yanatajwa kusaidia kupunguza magonjwa ya shinikizo la damu, na kwamba matunda aina hiyo husaidia pia kupunguza mawe kujaa kwenye figo.

Hivyo, inashauriwa kuwa ni vyema mtu akala tunda moja kwa wakati tofauti na sio kuchukua mengi na kuyachanganya ili kupata saladi. Tuifanyie kazi angalizo hili la Waziri Ummy kwa usalama wa afya zetu.

**SAFU**

**FIKRA MBADALA**

# Mabadiliko ya sheria bila mabadiliko ya Katiba ni sawa na kula bila kunawa



Pascal Mayalla

NILIPATA fursa kuhudhuria kongamano la siku tatu la vyama vya siasa nchini lililoandaliwa na Msajili wa Vyama vya Siasa nchini kwa lengo la kujadili ripoti ya Kikosi Kazi cha Rais Samia na mapendekezo yake kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 na Uchaguzi Mkuu wa 2025.

Kongamano hilo lilifanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Kwanza, ninampongeza Rais Samia kuunda kikosi kazi kutathmini hali ya siasa nchini. Ninakipongeza kikosi kazi kwa kazi nzuri na ninaipongeza serikali yetu kwa kukubali mapendekezo ya kikosi kazi, kukubali kufanya mabadiliko ya sheria ya uchaguzi na kurekebisha Tume ya Uchaguzi.

Kama ulitaka kikubwa, ukapewa kidogo, shukuru kwanza kwa hicho kidogo ulichopewa kisha endelea kuomba kile kikubwa.

Mzizi wa matatizo yetu yote ya uendeshaji wa siasa zetu, uko kwenye katiba kwanza ndipo tuje kwenye sheria.

Kufanya mabadiliko ya sheria bila mabadiliko ya katiba ni sawa na kula bila kunawa au kuvaa nguo nzuri bila kuoga. Ukila bila kunawa, utashiba tu, ila matokeo! Ukivaa nguo nzuri bila kuoga, utapendeza tu, ila...

Hivyo, ninaipongeza serikali yetu kukubali kubadili sheria, lakini ninashauri tuanze na mabadiliko ya Katiba ndipo twende kwenye sheria.

La pili; tufanye uchaguzi wote kwa siku moja, na kusimamiwa na tume moja huru ya uchaguzi. Kama Zanzibar wanaweza kufanya uchaguzi kwa siku moja, Tanzania Bara hatuwezi kushindwa kufanya uchaguzi kwa siku moja!

Hakuna haja ya kufanya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2024 halafu Uchaguzi Mkuu 2025, kwa sasa tufanye mabadiliko ya Katiba na sheria, halafu 2025 tufanye uchaguzi wote (serikali za mitaa, madiwani , wabunge na rais) kwa siku moja.

Kongamano hilo lilifunguliwa na Rais Samia ambaye alitoa wito kwa viongozi wa vyama vya siasa nchini kutumia mikutano ya hadhara kutoa hoja na fikra zenye tija zinazolenga kuimarisha utendaji serikalini.

Rais Samia pia alivitaka vyama vya siasa kutumia mikutano ya hadhara kujitangaza ili kukua kisiasa na kuutumia uhuru wa kujieleza kutoa mawazo mbadala yatakayoendelea kudumisha amani, umoja na mshikamano wa kitaifa.

Rais Samia pia alisema uhuru wa kutoa maoni usisababishe kudhalilisha watu wengine, kuibua hisia za kidini, ukabila au kubaguana kwa misingi yoyote ile.

Vilevile, Rais Samia alisisitiza kutumia uhuru huo vizuri bila kuingilia haki na uhuru wa watu wengine pamoja na kufuata sheria, kanuni na taratibu.

"Katika shukrani nisisahau Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, wakiongozwa na Jaji Mutungi, Jaji Mutungi saa zingine ananipigia simu usiku we mama wee hii kazi uliyonipa nimekwama hapa na hapa.

"Umeaminiwa kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa nenda na kazi yako, ukikwama fedha niambie lakini mengine fanya kazi yako. Kwahiyo, ninakushukuru umefanya kazi yako na mmefikia pazuri," alisema Rais Samia.

Alisema serikali imepokea ripoti ya kikosi kazi na imeyapitia mapendekezo hayo kupitia vikosi kadhaa vilivyongalia mambo kadhaa yanayohitaji wataalamu husasan yanayohusu sheria na Bunge lijalo, itapeleka marekebisho ya sheria kadhaa ikiwamo Sheria ya Uchaguzi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Rais Samia alisema kuwa kikosi kazi kimetoa mambo mazuri ambayo serikali kupitia wataalamu wake kwa kushirikiana na baadhi ya wajumbe wa kikosi kazi waliopendekezwa wamefanya mapitio ya mapendekezo hayo na kuja na namna bora zaidi ya utekelezaji.

Mwenyekiti wa Kikosi Kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demeokrasia ya vyama vingi vya siasa, Prof. Rwekaza Mkandara, akiwasilisha taarifa ya ripoti yao, alimpongeza Rais Samia pamoja na Rais Dk. Hussein Ally Mwinyi kwa juhudi zao za kuwaletea Watanzania maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii hususan kuboresha demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini.

Kwa vile msingi mkuu na matatizo makuu ya uendeshaji wa siasa zetu yako kwenye katiba, katiba ndiyo kichwa cha yote na mengine yote ni kiwiliwili.

Kwa vile kuna mchakato wa Katiba Mpya utakaoanza hivi karibuni, kwa minaajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa 2024 na Uchaguzi Mkuu wa 2025, tuanze na mabadiliko ya katiba hii hii iliyopo kwa kuibadilisha kwa hati ya dharura, ndipo tuje kwenye mabadiliko ya sheria za uchaguzi na kurekebisha Tume ya Uchaguzi tuunde Tume Huru na Shirikishi ya Uchaguzi.

**+255 754 270403**

**MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO**

# Watanzania tuache unafiki tuondokane na kadhia hizi



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

TANZANIA ni nchi tajiri sana! Tanzania ni nchi masikini sana! Hizi ni kauli mbili zinazosigana, zikitolewa na viongozi wengi wa nchi hii iliyopata uhuru wake Desemba 9, 1961.

Ni nchi ambayo ilipopata uhuru iliwekwa kwenye kundi la nchi za Dunia ya tatu, nchi masikini sana zilizohitaji misaada kutoka nchi za Dunia ya kwanza na ya pili.

Baada ya kubaki katika kundi hilo kwa kipindi kirefu, ikaonelewa yenyewe na mataifa mengine sawa nayo, yaingizwe kwenye mataifa yanayoendelea na si ya kundi la tatu tena.

Hivyo duniani kukawa na mataifa yaliyoendelea na yanayoendelea, na kumbe yaliyoendelea ni yaliyopata kuzitawala nchi hizi zinaoendelea, kabla ya kujipatia uhuru wao, nyingi ikiwa ni katika miaka ya sitini.

Kidogo kidogo katika kujinasua kutoka sifa hiyo, sisi mataifa haya tukaanza kulalamikia yaliyoendelea, kuwa yalinyonya rasilimali zetu na sasa yanaendelea kuzinyonya kwa maslahi yao, huku tukiambulia kidogo kupitia misaada.

Sasa wanaotuimbia kila siku kuwa Tanzania ni tajiri, ni hao viongozi wetu ambao wengi wanaogelea kwenye ukwasi huku sisi tukiimba kuwa Tanzania ni masikini, kwa kuwa tunaogelea kwenye umasikini.

Kwa miaka dahari tuliyojipatia uhuru, inashangaza bado tunakula mlo mmoja na kulala kwenye nyumba za tembe, bado hatuna maji ya uhakika wala umeme wa uhakika, tunazungumzia mgawo wa maji na umeme leo!

Lakini wakati hayo yanajitokeza, tunaona kabisa baadhi yetu wakiishi kwenye makasri na kutembelea magari ya kifahari, huku wenzetu sisi pangu pakavu tia mchuzi, tukikanyaga mbigili kuwatafutia wanetu maisha ya kesho yasiyo na uhakika.

Tunashuhudia wenye vinasaba vinavyofanana, wakipishana kwenye vyeo miaka nenda rudi na kutafutiana nafasi zenye hulua, huku wenye vinasaba vingine vinavyofanana pia, wakipishana mitaani kusaka shilingi.

Nchi inapopata uhuru huwa inajikomboa kutoka minyororo ya ukoloni na makucha ya mkoloni, hivyo kupata fursa ya kutafutia watu wake maisha mazuri, tofauti na ya utumwa na ukandamizwaji.

Ndiyo sababu hata wizara zinapoundwa, hulenga katika kuhakikisha hilo linatimizwa na wananchi wanafurahia uhuru walioukosa tangu kuzaliwa kwao katika nchi yao.

Ni nini basi kinatufanya Watanzania mpaka leo hatuna maji safi na salama na ya uhakika? Ni nini kinatufanya hatuna umeme wa uhakika wa kuendeshea mambo yetu ya kiuchumi? Kwa nini hatuna barabara na madaraja ya uhakika kila mahali?

Haya na mengine ni majibu yanayopaswa kujibiwa na tunaowapa dhamana ya kutuongoza, kutuwakilisha na kututetea. Je, wanafanya hivyo au wanapishana tu kwenye ofisi kubwa za nchi na kuranda na magari ya umma?

Tatizo linalotukabili Watanzania na husussan viongozi wetu, ni unafiki baina yao na yetu wenyewe, wanafanya hivyo kufurahishana, na huyu anafanya hivyo kuonesha yupo na anasaidia wananchi, lakini kumbe hakuna kitu.

Tunashuhudia baadhi ya viongozi walio na dhamira ya kweli, wakizunguka vijijini kufuatilia maisha ya watu waliosawajika na kutafuta ufumbuzi wa changamoto, lakini viongozi waishio na wananchi hujichekesha wawapo mbele za wakubwa zao ziarani na kumbe wakiondoka maisha husalia vilevile.

Mjengoni utaona wabunge wakitetea jambo kwa msimamo mmoja, kumbe kwa kuwa kuna kumulikana kwenye luninga na kusikika kwenye redio mbashara, watamridhisha mkuu wao, lakini wakitoka huko mgahawani wanamng'ong'a.

Tulishuhudia hili la mkataba wa DP World, baadhi wakikakamaa mishipa ya shingo kuitetea kampuni hiyo kuja kuwekeza, lakini nje ya hapo wanaongea kana kwamba hawakuwa wao waliokuwa wakitetea. Ni unafiki huo!

Hivi kweli tukikaa chini tukajiuliza, kulikuwa na haja ya kutumia fedha kibao kuhamishia makao makuu Dodoma kwa sasa na kujenga Ikulu ya zamani tena? Kulikuwa na haja ya kufufua Bwawa la Mwalimu Nyerere kuzalisha umeme sasa kwa kutumia maji licha ya mabadiliko haya ya tabianchi?

Kwani tungekataa kuyafanya hayo na mengine na watu kubaki Dar es Salaam, tungekuwa tumeshatoweka duniani? Hizo fedha zingetumika kuhakikisha maji safi salama na uhakika yanapatikana, umeme wa uhakika unapatikana.

Tangu awamu ya nne ya uongozi wa nchi hii, tulishagundua gesi Mtwara na kuhanikiza kuwa itazalisha umeme na ziada kuuza nje, lakini mpaka leo bila aibu tunazungumzia mgawo, kweli? Kwani tungesimamia hapo leo tungelia na umeme?

Kwa nini sasa nguvu zisielekezwe kwenye gesi katika kipindi hiki ambacho petroli na jamaa zake bei inapanda kila siku? Tunaimba tunahamia kwenye gesi hata magari yatumie gesi, lakini tuna vituo viwili tu vya kujazia gesi kwenye magari? Tuko makini kweli au unafiki?

Kila mmoja wetu anashudia mama wa watu, Chifu Hangaya anavyohaha ndani na nje ya nchi kututafutia maisha mazuri, lakini wanafiki wanamkwamisha na kuhanikiza majukwaani "Samiya Oyeee! Samiya Oyeee! Tumwombee maisha mema!" Unafiki mtupu! Mungu anakuoneni Walahi!

# Barabara mpakani Tanzania na Malawi mbioni kujengwa

**Na Moses Ngw'at**, ILEJE

SERIKALI imewalipa Sh. milioni 850 wananchi watakaopisha ujenzi wa barabara ya lami kutoka Isongole wilayani hapa hadi Kasumulu Kyela Mkoa wa Mbeya.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Godfrey Kasekenya, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Bupigu akiwa katika ziara yake ya kikazi wilayani Ileje, alisema ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 124 unatarajia kuanza hivi karibuni baada ya kupatikana mkandarasi.

Kasekenye alisema ujenzi huo utaanza kwa kilometa 52 kutoka Isongole hadi Ndembo - Isoka wilayani Ileje baada ya wananchi hao kulipwa fidia.

Alisema lengo la serikali kujenga bararaba hiyo ni kuboresha miundombinu ya mawasiliano ya barabara na kukuza uchumi wa nchi na Watanzania.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo ni muhimu kwa Tanzania kwa sababu itaiunganisha na nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kusafirisha mizigo.

Alitaja umuhimu mwingine wa barabara hiyo kuwa ni ya ulinzi kati ya Tanzania na Malawi.

"Barabara hii pia ni ya kimkakati kwani itasaidia kusafirisha shehena ya makaa ya mawe kutoka kwenye mgodi wetu wa Kiwira na itasadia kuifungua nchi kutoka mikoa ya Kusini hadi Magharibi kisha kwenda nchi za Burundi na Kongo (Jamhuri ya Kidemokrasia Kongo (DRC)), " alisema Kasekenya.

Amewataka wananchi wanaotakiwa kupisha ujenzi wa kipande cha pili cha barabara hiyo kuanzia Ndembo wilayani Ileje hadi Ngana kwenda Kasumulu kutoa ushirikiano kwa wataalamu watakaofika katika maeneo yao kufanya tathamini ya mali zao.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Songwe, Suleiman Bishanga, alisema taratibu za kupata mkandarasi wa ujenzi wa barabara hiyo kutoka Isongole hadi Ndembo kwenda Isoko umeanza.

# NGO zatoa kitabu chenye malalamiko dhidi ya TRA

**Na Thobias Mwanakatwe**, DODOMA

MASHIRIKA yasiyokuwa ya kiserikali (NGO) yametakiwa kuwatumia wahasibu waliosajiliwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA) kuandaa hesabu kwa usahihi ili kujenga hoja za kujitetea kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhusu kodi wanazozilalamikia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Filadefia inayojishughulisha na utoaji wa mafunzo ya uhasibu, Janjason Kibona, alitoa ushauri huo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa kufuatia NGO'S kuandaa kitabu chenye malalamiko 25 dhidi ya TRA kuhusu kodi wanazotozwa kwenye jukwaa la mwaka la mashirika hayo.

Alisema NGO zikiwa zinawatumia wakaguzi wazuri kutoka NBAA kutakuwa na hesabu nzuri na kuwatetea kwenye kodi kwa sababu kutakuwa na ushahidi kwa yule anayekudai.

"Wafadhili wengi ambao wanatuletea fedha sisi NGO ni serikali za nchi nyingine, mfano jana tuliona mwakilishi wa Umoja wa Ulaya akieleza wao wanapopewa fedha kuja katika hizi NGO na wenyewe wanakaguliwa, sasa inapoonekana 'financial statement' haziko sawa maana yake tatizo hilo linaweza kuwa kubwa na kukosa hiyo misaada," alisema.

Kibona, alisema ushauri mwingine anapotoa kwa NGO kuepukana na usumbufu ni kuwawezesha wahasibu kushiriki mafunzo maalum yaliyoandaliwa na Bodi ya NBAA kama ambavyo serikali imekuwa ikifanya ili kuimarisha ufanisi na utendaji kwa sababu kanuni za kuandaa hesabu zinabadilika kulingana na dunia inavyosonga mbele.

"Kama NGO zitajikita kuwa na wahasibu ambao wamebobea katika uandishi wa hizi hesabu wanaweza kuwa na hoja nzuri ambapo hata maandiko yao wanapoomba fedha kwa wafadhili yatakubaliwa na pia wanapokwenda TRA wanakuwa na pa kuzungumzia," alisisitiza.

Aliitaja njia nyingine ya kuzisaidia NGO kuwa ni kuwatumia washauri ambao wamesajiliwa na TRA kama mawakili wa kushughulikia mashauri yao ya kodi kwa sababu suala la kodi ni la kisheria.

Kibona, alisema kuna NGO wajumbe wake ni wabunge kwa hiyo waanzishe mchakato bungeni wa mabadiliko ya sheria zibadilishwe ili kuzisaidia zijiendeshe vizuri.

"Huwezi kulalamika kuwa sheria ziondoke hivi hivi mdomoni unatakiwa upeleke hoja bungeni ya kubadilisha sheria inaweza kufanyiwa kazi haraka," alisema.

Alisema katika kitabu chenye malalamiko 25 kilichoandikwa na NGO, zinajenga hoja kwamba zinafanya kazi ya kutoa huduma kwa jamii kwa kutumia fedha za kodi za serikali nyingine.

Kibona, alisema TRA ina kitu kinachoitwa 'service Charter'ambayo inaonesha mkataba wake na mlipakodi ambao ndani yake kuna wajibu wa mamlaka hiyo katika kutenda kazi za kodi, pia kuna wa NGO.

"Huu mkataba ndio mzuri ili kuepuka wapi ni wapi na hili likifanyika panaweza kufanyika suluhu ya malalamiko kwani sheria za nchi zipo wazi kwamba NGO kama taasisi binafsi zinapaswa kuandaa hesabu sahihi kwa kuwatumia wahasibu sahihi," alisema.

Kibona aliongeza kuwa tangu mabadiliko ya sheria yamefanyika mwake 2019 kwa ajili ya kutengeneza mambo mazuri ya kisheria ya kusimamia NGO, NBAA ilitoa mwongozo kwamba mashirika hayo yanaweza kuandaa hesabu zao kwa uwazi.

Alisema malalamiko mengine ya NGO nyingi yanagusa suala la elimu na kushauri TRA iwe inatoa elimu kwa mashirika hayo kwa kuwatumia mameneja wa mikoa wa TRA katika mikoa husika ili kuondokana na malalamiko kwamba hazipewi elimu.



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba (kulia), akikabidhi cheti cha shukrani kwa Ofisa wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Wilaya ya Kinondoni, Zuwena Abdallah, kwa ushirikiano walioutoa wakati wa Wiki ya Huduma kwa Wateja mwaka 2023, Dar es Salaam juzi. Wengine ni Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Mfuko huo, Mbaruku Magawa (wa pili kushoto) na Meneja wa Kanda wa PSSSF Kinondoni, Ritha Ngalo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Exim yaadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja, ikiahidi huduma bora

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim nchini imeungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja 2023 chini ya kaulimbiu ya 'Team Service' huku ikirejelea dhamira yake ya kuendelea kutoa huduma zinazokidhi matakwa ya wateja, ambayo ni moja ya misingi ya benki hiyo.

Wakati wa hafla ya uzinduzi wa mwezi wa huduma kwa wateja wa benki hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Exim, Jaffari Mtundu alisema huduma kwa wateja ni miongoni mwa miiko na utamaduni wa benki yake.

Matundu alisema kaulimbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka huu ya 'Team Service' inaendana hasa na falsafa ya Exim ya kuongeza huduma wateja kwani ni chachu ya biashara na imeweka kipaumbele cha huduma kwa wateja.

"Hii ndiyo sababu Benki ya Exim inaendelea kuwekeza mara kwa mara katika teknolojia na kuwapa wafanyakazi wetu ujuzi na rasilimali zinazohitajika ili kuhakikisha wanawapa wateja wetu huduma za hali ya juu," alisema.

Alisema benki hiyo imetoa kipaumbele kwa mteja kwanza kama njia bora ya kutoa huduma ya kipekee hali ambayo inasaidia kuuza bidhaa na huduma za benki hiyo.

Matundu alisema benki hiyo mwanzoni mwa mwaka huu iliboresha mfumo na kuweka miundombinu thabiti, hatua inayolenga kuimarisha utendaji na kuwapa wateja usalama, ufanisi na uvumbuzi.

"Hii inadhihirisha ari yetu katika kubadilika na kuwa zaidi ya taasisi ya benki.

Kama benki, tumejitolea kuwekeza katika kuongeza uwezo wa mifumo yetu ili kutoa huduma bora kwa wateja na jamii inayotuzunguka.

Lakini nina hakika faida ya ushindani katika benki itatokana na teknolojia inayoendeshwa na watu.

Kama benki, hatuna chaguo ila ni kuendelea kuwapa wateja wetu thamani zaidi katika utoaji huduma," alisema.

Aliipongeza idara ya huduma kwa wateja ya benki hiyo na wateja wake kwa kuendelea kuwa wafadhili na kujitolea kwa chapa ya Exim, na kuwahakikishia itaendelea kukidhi mahitaji na kuvuka matarajio kwa kutoa bidhaa na huduma bora.

Mkuu wa Idara ya Huduma kwa Wateja cha Exim, Frank Matoro, alisema benki hiyo itaendelea kuwekeza kwa wateja wake katika masuala ya ujuzi ili kuhakikisha wanatoa huduma bora.

# MAISHA

OKTOBA 8, 2023

**Nipashe**

**Baba, Mama na Mwana**

*Jumapili*

Ukurasa 14




## Kunywa juisi ya nanasi upendavyo

## MAISHA NI NYUMBA

Ukurasa 15



Uchafu unaharibu nyumba, panga ratiba nzuri kuisafisha




## KATUNIKA


Ukurasa 16



# KUWA HURU UFUKWENI

Ukurasa 13

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



Majina ya Wanafamilia
**MJOMBA, BABA**


Majina ya Vyombo vya Usafiri
**MELI, GARI**

Majina ya Vifaa vya Shule
**DAFTARI, PENI**

Majina ya Mifugo
**KUKU, SUNGURA**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | ■ | O | M | B | W | A |
| C | ■ | ■ | ■ | W | ■ | C |
| H | ■ | F | A | A | ■ | H |
| A | D | A | ■ | T | A | A |
| N | ■ | G | O | A | ■ | N |
| G | ■ | I | ■ | ■ | ■ | G |
| O | G | O | P | A | ■ | I |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

MBU, MEI, DAU, BEI, MBUGA, AMANA, UGUMU, DIMBA, SHABAHA, ANZISHA

## TOA TOFAUTI 5



## AMSHA AKILI

ILI KUJUA MBWA ANASEMA NINI, FUTA HERUFI L ZOTE.




## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

MTOTO john alikuwa akitembea na mama yake, mara aliwaona watu wakiwa chini ya mti mmoja akimnyoa nywele mwenzake.

Baada ya kuwaona wale watu John alianza kulia huku akizishika nywele zake.

Mama: John unalia nini mwanangu, mbona tulikuwa tunatembea vizuri?

John: Mama mwalimu alituambia ukiona mwenzako ananyolewa, wewe tia maji nywele zako

Mama: Sasa kinakuliza nini hapo, si msemo tu huo?

John: Yule anayenyolewa ni rafiki yangu darasani, akimuona mwalimu kanyoa na mimi atataka ninyoe

Mama: We John huo ni msemo tu, mwalimu wako anamaanisha kinachompata mwenzako kinaweza kukupata na wewe.

John: Kumbe

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mimba ya nje, anakunywa sumu kisa mume kaoa mke mwingine!

KARIBU tena msomaji tuendelee kusikia vituko vya Maisha Ndivyo Yalivyo. Hebu sikia hii:- "Yupo mama, mke wa mtu ana uhusiano na mwanamume mwingine wa nje na inasadikika huyo ndiye aliyempa ujauzito alio nao hivi sasa.

"Siku aliposikia mumewe kaoa mke mwingine (kama dini inavyoruhusu), huyu mama alitaharuki na kwenda dukani kununua sumu ya panya na kuinywa, hali akiwa na ujauzito.

Msimulizi wangu anasema, "ndipo nikashangaa ana maana kuwa anampenda sana mumewe? Au vipi! Mbona ana ujauzito wa mtu mwingine? Sijajua huyu mama ana mapenzi ya aina gani".

Mpenzi msomaji, ama kweli Maisha Ndivyo Yalivyo. Mwanamama anayedaiwa kubugia sumu ya panya akijaribu kujiua alifanya hivyo wakati akiwa na mimba ya mwanamume wa nje ya ndoa.

Hata hivyo, dini inambana yule mwanamume wa nje kumdai mtoto huyo endapo itathibitika kuwa ni wake kutokana na msemo uliozoeleka kuwa kitanda hakizai haramu.

Hata kama ni wivu kwa mumewe kuoa mke mwingine, mbona yeye amevunja uaminifu na kuwa na uhusiano na mwanamume mwingine?

Ni dhahiri kwamba mke huyu aliyetaka kujiua hana uvumilivu, hana uaminifu, ana wivu wa kijinga huku akijua kuwa mumewe dini inamruhusu kuoa mwanamke zaidi ya mmoja.

Kama kweli alilijua hilo, kwanini yeye (mama) aamue naye kuwa na mume zaidi ya mmoja nje ya ndoa wakati kwa upande wa wanawake hairuhusiwi? Kama alitaka mwanamume mwingine, ilitakiwa aombe talaka, akubaliwe, kisha akajiegemeze kwa huyo mwanamume mwingine wa nje. Au siyo?

Hili ni tatizo kubwa sana katika familia zetu nyingi, kwa baadhi ya wanawake kutaka kushindana na mumewe kwa kila jambo alifanyalo. Ni vyema kinamama wakatambua kuwa siyo kila jambo linahitaji kufanyiwa ulinganifu/ushindani. Mengine ni asili na yanapaswa kuheshimiwa.

Ni muhimu ikaeleweka pia kuwa mwanamume kuacha na kuona mwingine ni rahisi sana kuliko mwanamke kuachwa na kuolewa tena. Mwanamke anayejulikana kuwa alishaolewa kisha akaachika, wengi thamani yao hushuka kulinganishwa na mwanamume aliyeacha na kuoa tena.

Hebu turejee kidogo kisa cha hapo juu, mwanamama aliyetaka kujiua kwa sumu wakati anaye mumewe ndani, lakini bado anamtamani mwanamume wa nje. Inawezekana ni wivu kwamba alizoea kuwa peke yake ndani, lakini sasa mumewe amejigawa kaoa mwingine, kwahiyo penzi limegawanyika.

Pengine anajiona mpweke mumewe anapokuwa kwa mke mwenzake, ndipo anashawishika kula kona kwa mwingine. Anasahau huko nako kuna karaha zake, uhusiano ukakolea na bila kujua mimba ikanasa. Akadhani mimba ni ya mume kumbe sura itatoboa siri.

Kisa hiki kinanikumbusha ripoti moja iliyowahi kutolewa na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali nchini kuhusu kinababa wengi hubambikizwa watoto. Ripoti hiyo ikasema kuwa zaidi ya asilimia 48 ya wanaume waliojitokeza kupima vipimo vya vinasaba (DNA) waligundulika kubambikwa watoto.

Takwimu hizo za vipimo vya DNA zilichukuliwa ndani ya miaka mitatu. Ni ripoti iliyotolewa jijini Dar es Salaam mwaka 2010 na Ofisi ya Uchunguzi wa Vinasaba ya Mkuu wa Kitengo cha Makosa ya Jinai na Vinasaba vinavyotokana na matukio na mashauri mbalimbali.

Ikaonesha asilimia 48.32 ya watoto waliofanyiwa vipimo vya DNA kwa kipindi hicho waligundulika hawalelewi na baba halali. Kwenye utambuzi wa uhalali wa watoto, sampuli mbalimbali kutoka kwa watu tofauti zilizopimwa zilionyesha asilimia kubwa ya watoto hawalelewi na baba halali.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, idadi hiyo ni kubwa watoto walioonekana hawana uhalali wa vinasaba vya mzazi wao (baba), lakini takwimu hii siyo kwa nchi nzima ila tu kwa wale waliofika ofisini kutatua mashauri ya kufahamu watoto wao.

Kwa kutumia teknolojia hiyo, sampuli za wazazi na watoto huchukuliwa na kuingizwa katika mashine yenye uwezo wa kuchambua vinasaba na kugundua uhalali wa mtoto. Vinasaba vina umbo la majimaji yenye kemikali, ambayo yana taarifa kamili ya mtu husika ikiwa ni asili yake, umbo, rangi na jinsia.

***Usikose sehemu ya pili ya mada hii Jumapili ijayo. Mume, mke washindana kuzaa nje ya ndoa. Je, una maoni, kisa cha kimaisha ungependa tujadili pamoja? Ukiwa tayari tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Bila sheria ndogo vijijini, hakuna nguvu kazi ya taifa

USIMAMIZI ni kufanya jambo kwa usahihi, lakini uongozi ni kufanya vitu sahihi. Ndiyo!

Kuna mambo matatu ninayatazama hapa ambayo ili kulinda maadili yetu tunapaswa kuyazingatia. Moja ni taadhima, yaani kile tunachopaswa kuonesha na kuonesha wale tunaowahudumia bila kufeli.

Pili, uadilifu ni msingi mkuu wa kila tufanyacho, na tatu ni suala la ujumuishaji, ambalo ni msingi wa kupatia watu kipaumbele kwa kila tufanyacho.

Hakuna shaka kwamba, katika mfumo wetu wa maisha, huwa ni jambo la kawaida mtoto kutunzwa au kulelewa na wazazi/walezi kwa kuzingatia malezi na makuzi yanayoshajihi maadili mema.

Lakini hivi sasa kukosekana kwa maadili ndani ya jamii kunatajwa kama moja ya vyanzo vya kushamiri vitendo vya ukatili vinavyowaathiri wanawake na watoto kwa kiasi kikubwa.

Siku zote ukiona jamii inaukataa ukweli iache. Ukweli haujawahi kuwa rafiki wa dunia hii. Wakweli wameangamizwa na dunia katika umri mdogo wa miaka 30 na kuendelea. Mfano mzuri ni Yesu Kristo, aliyeuawa na kutundikwa msalabani akiwa na umri wa miaka 33, mpigania haki, Martin Luther Junior miaka 37 na Mwanafalsafa Che Guavara, alipoteza maisha akiwa na miaka 39.

Ninataka kusema nini. Nimevutiwa uamuzi wa viongozi wa Serikali ya Kijiji cha Olevolos kilichoko Kata ya Kimnya, Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, kutunga na kupitisha adhabu kali inayowabana vijana wanaoshinda vijiweni kutwa nzima wakiwa hawana kazi.

Kwamba wakati changamoto ya mmomonyoko wa maadili ikizidi kuchukua sura mpya kila siku ndani ya jamii, wananchi wanaazimia kuanzia sasa, watakaokamatwa vijiweni bila kazi maalum, watalazimika kulipa faini ya Sh. 50,000, na kama hana atapelekwa kwenye baraza la wazee kupatiwa adhabu mbadala.

Wamekwenda mbali zaidi, wametangaza marufuku nyingine ya kuzuia vijana wa kiume kusuka nywele au kunyoa pembezoni mwa kichwa na kuacha katikati (kiduku) au kuvaa suruali mlegezo, inayoonyesha makalio au aina ya suruali iliyotobolewa (crazy jeans).

Kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kimnyaki, Joshua Mollel, faini yake ni Sh. 50,000 na kama huyo kijana hana, kuna adhabu nyingine ambayo wazee wamependekeza.

Wananchi wa Olevolos hawana tofauti na vijiji vingine vya Meru, ambao nao walipitisha sheria ndogo ya kudhibiti vitendo hivyo vya mmomonyoko wa maadili.

Kimsingi, makali ya sheria hiyo ndogo pamoja na mambo mengine, pia yanazuia msichana au mwanamke yeyote kuvaa suruali ya kubana na kuonyesha maungo yake au sketi fupi, maarufu kimini.

Kwamba wewe mwanamke au msichana, ukibainika faini yake ni Sh. 50,000 na kama hauna, kinamama wako walioandaliwa, watakushughukia kwa adhabu mbadala.

Na ni marufuku kijana kuonekana amevaa hereni, ukikutwa adhabu yake ni Sh. 50,000 na kama hauna, wazee wapo. Watakushughulikia!

Vilevile, katika sheria hiyo kuna marufuku ya kulewa au kuuza pombe saa za kazi. Ukikamtwa, adhabu yake ni faini ya Sh. 50,000. Huu ni mkakati mahususi, ninaounga mkono utumike kwenye vijiji vyetu.

Mja ni vitendo na muungwana ni vitendo. Sina budi kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima kwa kuunga mkono uamuzi wa wananchi kutunga sheria ndogo inayolenga kuzuia mmomonyoko wa maadili na kudhibiti janga hilo kwenye eneo lao.

Dk. Dorothy amesema jitihada hizo za kukabiliana na mmonyoko wa maadili ni hatua kubwa kwa jamii yetu, kubeba ajenda za kusaidia jamii kwenda mbele hasa katika maadili, fursa za kiuchumi na kupinga ukatili.

Wananchi wenyewe kumiliki ajenda ya kupambana na mmonyoko wa maadili ni mfano wa kuigwa na kila mtu.

Ni rai yangu na kwa serikali yetu au jamii yote kwa ujumla kuendelea kuunga mkono juhudi za viongozi na wataalamu wa serikali ngazi zote katika kupambana kutokomeza ukatili wa kijinsia na watoto pamoja na kudhibiti mmomonyoko wa maadili kwa ujumla.

***Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe Kanda ya Kaskazini.**
**Barua pepe: ghandsome79@gmail.com**
**Simu ya mkononi: +255 767 535490***

# HARUSI







Ilikuwa siku ya furaha Boniphace Bwire Mateko na Regina Mbwambo Msifuni baada ya kufunga ndoa Septemba 10, mwaka huu katika Kanisa la Wasabato Bomani mjini Bunda mkoani Mara. Sherehe ya kuwapongeza ilifanyika katika ukumbi wa Malaika Resort mjini humo.



# MITINDO

## KUWA HURU UFUKWENI

KIPINDI cha joto kimewadia, kila mtu anahitaji kupata hali ya hewa ya baridi ili kuupoza mwili.

Sehemu inayopendwa na wengi kwenda kutuliza joto mwilini ni maeneo ya fukwe za bahari. Maeneo haya yanakuwa na upepo mwanana unaofanya mtu kupata tulizo la mwili.

Hata hivyo, kuna aina ya mavazi ambayo unashauriwa kuvaa hasa kutokana na urahisi wa kufanya mambo mengi kwa wakati mmoja.


Vazi la kaptura nyepesi linapendekezwa zaidi kutumika endapo unataka kwenda kupunga upepo ufukweni.

Aina hii ya nguo itakurahisishia kupata hewa vizuri, kuogolea majini na kufanya matembezi ya ufukweni bila kupata usumbufu.

Kwa wale wanaopenda kuvaa nguo ya juu, si vibaya kama utakuwa na fulana au shati jepesi. Lakini kwa wanaume kama sehemu ya juu ya mwili ukiwa wazi ni vizuri zaidi.

Kama umejipanga vizuri unaweza kubeba pia nguo za kuogelea kwani itasaidia kuwa na chaguo zuri kila unapotaka kufanya kitu.

Upande wa viatu, unashauriwa kuvaa viatu vyepesi kama sando, raba au viatu vya wazi vilivyotengenezwa kwa plastiki laini.




URFEMBO

## UREMBO

**Na Mary Geofrey**

# MAAJABU YA YAI kwenye ngozi, nywele



YAI limekuwa likitumika zaidi kama chakula muhimu kwa muda mrefu, wapo wanaokula kwa kukaanga, kuchemsha, kunywa likiwa bichi au kuchanganya katika vyakula vingine.

Hata hivyo, kuna matumizi zaidi ya yai kutokana na kuwa na uwezo mkubwa wa kurutubisha ngozi, nywele na pia kuondoa uchovu.

Ukitaka kutumia yai kuboresha muonekano wa ngozi na nywele zako unatakiwa kufanya yafuatayo.

Chukua yai, changanya na asali kijiko kimoja cha chai mafuta ya mzaituni.

Chukua mchanganyiko huo kisha pakaa usoni na shingoni, kaa nao kwa dakika kumi hadi 15.

Hii itasaidia kuondoa mashimo usoni yatokanayo na chunusi. Pia hulainisha ngozi yako na kuwa nyororo.

Mchanganyiko huu pia utasaidia kuondoa michubuko au alama za kuungua na jua, mafuta au matumizi ya kemikali.

Unaweza kutenganisha kiini cha yai na ule ute mweupe, kisha chukua ute weka kwenye kikombe au bakuli, baada ya hapo pigapiga ule ute hadi uwe na mapovu kisha chukua povu na nawa usoni au paka mwili mzima kisha liache likauke.

Baada ya hapo osha kwa maji ya uvuguvugu, ukifanya hivyo mara kwa mara itakusaidia kufanya ngozi yako iwe angavu.

Kama umetoka kazini na unaonekana umechoka na unataka kutoka usiku, chukua ute wa yai na pakaa chini ya jicho na uache kwa dakika 10 hadi 15 kisha safisha, itasaidia kuondoa muonekano wa uchovu katika macho yako.



## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Kunywa juisi ya nanasi upendavyo

FAIDA za juisi ya nanasi katika mwili ni kusaidia mmeng'enyo wa chakula, kupunguza uzito na kuharakisha tishu na uponyaji haraka wa ngozi.

Unaweza kutumia nanasi kwa kusaga yenyewe au ukachanganya na matunda mengine.

**Nanasi na Pesheni**

Hii ni kwa wanaofurahia vinywaji vyepesi na ambavyo vina uchachu kwa mbali, unachohitaji kutumia nanasi limeiva vizuri na kuchanganya na pesheni mbili za ukubwa wa wastani.

Menya nanasi kisha kata vipande vidogo vidogo na weka kwenye blenda. Kata karakara kisha weka tunda zake kwenye kikombe tofauti kama hautotaka kuchuuja juisi yako.

Anza kusaga nanasi weka kwenye jagi na kisha saga pesheni na uchuje peke yake na uichanganye na ile ya nanasi ambayo haijachujwa.

Kama utachuja juisi yako ya nanasi, changanya matunda yote kwenye blenda na usage kwa pamoja na juisi yako itakuwa tayari

Nanasi na ndizi

Mchanganyiko wa nanasi na ndizi ni wa aina yake.

Siyo lazima nanasi liwe chachu,hata likiwa tamu bado unaweza kutengeneza juisi hii.

Wakati nanasi ikikupatia nyuzi nyuzi, ndizi huchochea usingizi, husaidia kinga ya mwili na pia inatajwa kupunguza msongo wa mawazo.

Nanasi na maji ya dafu

Baadhi ya watu hupata ugumu kunywa maji ya nazi, lakini ukichanganya na

nanasi utapata faida nyingi ikiwamo kuongeza nguvu kwa wanaofanya mazoezi na kuchochea mmeng'enyo wa chakula.

Pia juisi hii inasaidia kuchochea mlinganyo wa hisia (mood) huku kwa wanaopenda ngozi zao, ikiwapatia mng'aro wa aina yake.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Uchafu unaharibu nyumba, panga ratiba nzuri kuisafisha

UCHAFU unachangia kwa kiwango kikubwa kuharibu nyumba hata kama ni nzuri na iliyojengwa katika uimara mkubwa.

Mwingine anaweza kusema 'mbona kusafisha nyumba ni jambo linaloeleweka?' Ninachotaka kueleza ni namna gani unatakiwa kuweka kipaumbele na kujiwekea ratiba nzuri ya usafi wa nyumba yako yote.

Na kumbuka kwamba nyumba ikisafishwa kwa umakini na ufasaha ni dawa inayojitosheleza katika kuiimarisha na ikadumu zaidi kama ambavyo ni kinyume kwamba isiposafishwa vizuri ina uwezekano mkubwa wa kuharibika na kupoteza mvuto na uimara wake.

Jambo la msingi na la kuzingatia ni kwamba, nyumba ina maeneo mengi na kila eneo linahitaji kusafishwa kwa umakini kwa ajili ya ustawi wake.

Ili ufanikiwe katika hilo ni lazima kujiwekea utaratibu mzuri wa kujipangia ratiba ya namna gani bora ya kufanya usafi katika kila eneo la nyumba yako.

Kwa mfano kama ni jikoni, chumbani, sebuleni, jikoni, nje ya nyumba, stoo, vyooni na katika viunga vyote vya nyumba hakikisha kwamba kote kunafanyiwa usafi wa uhakika kila mara.

Kwenye maeneo yote ya wazi yakiwamo yale yanayohitaji kufagiwa, hakikisha unafanya hivyo. Kama umepanda maua, yahudumie nayo vizuri kwa kuyawekea mbolea na kuyamwagia maji pamoja na kuyatengenezea mazingira ya kuendelea kustawi zaidi na yasigeuke kuwa uchafu kwenye nyumba.

Na baada ya kufanya usafi hakikisha unakagua kila eneo la nyumba ili kujiridhisha kama endapo kila mahali kumeguswa na usafi na kama kuna vitu ambavyo havihitajiki au havitumiki, viondoe.

Na baada ya kusafisha hakikisha kila kitu kwenye nyumba kimepangwa inavyostahili kuanzia jikoni, sebuleni, vyumba vya kulala, vyooni na hata nje ya nyumba kwenye bustani na sehemu nyinginezo.

Hakikisha kwamba yale maeneo yote ambayo yanahitaji kufanyiwa usafi kila siku inafanyika hivyo na usafi kwenye kila eneo la nyumba yako ndio utaiimarisha. Endapo hakutakuwa na mpango mzuri wa kuisafisha utaiharibu.



# Mapambo ya asili yanaleta unadhifu ndani

**Na Restuta James**

MAPAMBO asilia yanayotokana na miti yaani mbao, fito, magome na makuti vinavyotengenezwa kwa mikono, vinaendelea kushika kasi ya mapambo ya ndani barani Afrika na nje ya bara hili.

Mtaalamu wa mapambo ya ndani, Jenna Kate, katika chapisho lake la wiki hii anasema aina hiyo ya mapambo haipitwi na wakati akieleza changamoto yake kubwa ni bei kwenye nchi zilizoendelea.

Anataja mapambo hayo kuwa ni viti, meza, stuli na mito; ambavyo vinaweza kutumika ndani ya nyumba na bustanini.

Anasema samani hizo zipo pia kipande cha gogo kinachoweza kupolishiwa na kubakia na mwonekano wake wa asili kisha kutumiwa kama meza ndogo sebuleni au bustanini.

"Aina hii ya meza ni moja ya bidhaa zinazouzwa sana mtandaoni kutokana na mwonekano wake kuleta uhalisia na uhai ndani ya nyumba," anasema Jenna.

Anafafanua kuwa ziko meza nyingine zinazotengenezwa kwa fito ndogo zikiwa na umbo la ngoma, zinazoongeza mvuto ndani ya nyumba.


Anasema vitu asilia kama mbao na fito vinatumika pia kutengeneza 'holder' ya taa, ambayo itakamilisha seti ya vitu asilia ndani ya nyumba kwa mtu ambaye ameamua kutumia mapambo ya asili.

Kingine ni fremu ya kioo ambayo nayo inaweza kutengenezwa kwa kutumia mbao badala ya aluminiamu au chuma.

"Ukifuatilia masoko makubwa mitandaoni utabaini kwamba hizi ni samani zinazouzwa zaidi japokuwa bei yake kubwa ni changamoto," anasema.



## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
NIMNUNIE NANI WAKATI MAISHA NIMEYAKOSEA MWENYEWE KAMA HESABU ZA 'MARA NA JUMLISHA'
JUKWAANI
MILO MITATU
"AMMA!"
UMEMTUSI WAIFU WAKATI WE'KIMADA HUJULIKANI POPOTE! 'NIMEKUTEMA'
TAFUTA SABABU AU KWA KUKUSAIDIA NAKWENDA KUMZABA VIBAO!
MPAKA JIONI MKONO KAMA NIMESHINDA 'JIMU'
KAMA UNAKATAA HUJAIANDIKA HII TALAKA MBONA MWANDIKO NI WAKO?
HIYO NI KAZI YA POMBE SIO MIMI BABA MKWE!
UNAMTETEAJE BODABODA WAKATI AJALI AMEJITAKIA?
YULE BHANA HAPONI! MTU GANI ANA-ONGEA UBONGO 'UNAMWAIKA!' ALAFU TENA WANATANATA!
UBINADAMU UNAHITAJIKA YULE NI MTU
ALIYESEMA YULE NI BATA NANI?
AWE MTU AU BINADAMU HAKUTUMWA KUWA MZEMBE BARABARANI
WAJA LEO OYEE!
MBONA WENZIO MATAJIRI?
SASA RAHA IKO WAPI? NINGEWEZAJE KUTAFUNA MIGUU YA KUKU BARABARANI!
MONDE BHANA IKIKUREMBULIA HUKUMBUKI KAMA NI MUME WA MTU!
UTAZIVAA MWENYEWE WAMEGOMA KUNUNUA!
AFADHALI MIMI LAKINI HIZO ZAKO ZA KIKE PATA PICHA 'UKIZITINGA'
*KINYUNYIZO CHA LEO...
MUHESHIMU SHEMEJIO DADAAKO KAOLEWA...

# KUPATWA KWA ISRAEL

## -Wapalestina washambulia kila kona
## -Wadai kuteka wanajeshi, kifaru, gari





**TEL-AVIV, ISRAEL**

DUNIA imeshtushwa baada ya wanamgambo wenye silaha kutoka kundi la wapiganaji wa Palestina Hamas kujipenyeza kusini mwa Israel kutoka Ukanda wa Gaza na kufanya mashambulizi makali.

Jumla ya watu 22 wameuawa na wengine kadhaa wamejeruhiwa katika mapigano hayo, huku ikiyaacha baadhi ya majengo yakiwaka moto katika mji mkuu wa Tel Aviv.

Kulingana na picha za video zilizosambaa katika mitandao ya kijamii kuanzia jana asubuhi, ilionekana wanamgambo hao wakifyatua risasi na kurusha maroketi kuelekea Israel.

Wanamgambo hao walianza kutekeleza mashambulizi yao katika mitaa ya mji wa Sderot nchini Israel.

Katika kilichowashangaza wengi, wanamgambo hao walifyatua roketi kali kutoka Gaza na kulenga makazi ya watu nchini Israel na pia ilimuua mwanamke mmoja wa Israel.

Waziri wa Ulinzi wa Israel, Yoav Gallant alisema Hamas imefanya makosa makubwa na kuanzisha vita dhidi ya nchi yake.

"Wanajeshi wa Israeli wanapambana na adui katika kila eneo, taifa la Israel litashinda vita hivi" alisema Yoav Gallant.

Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) lilisema limehamia kwenye kituo cha vita na kwamba ndege za kivita zilikuwa zikifanya mashambulizi ya anga kwenye maeneo ya Hamas katika ukanda wa Gaza.

Video za kutisha zinazosambazwa kwenye mitandao ya kijamii zinawaonyesha wanamgambo wa Kipalestina wakiwafyatulia risasi wapita njia katika mitaa ya kusini mwa Israel.

Kuna ripoti kwamba baadhi ya nyumba zimetekwa na watu wenye silaha mjini Sderot kutoka kundi la Kiislamu la Hamas, ambalo linatawala Gaza.

Jeshi la Israel liliwatangazia wakazi wa eneo hilo kusalia majumbani mwao kufuatia ripoti za kujipenyeza kwa wapiganaji hao.

Mashambulio makali ya roketi na makombora ya masafa marefu yalianza kuanzia alfajiri katika hali ya kushtukiza na kuwafanya walinzi wa Israeli kukimbia.

Aidha, moto mkubwa umeshuhudiwa ukiwaka katika maeneo ya kusini mwa Israel ambako roketi zimekuwa zikilenga.

Kamanda wa ngazi ya juu wa jeshi la Hamas alitangaza kuanza kwa operesheni hiyo katika matangazo kwenye vyombo vya habari na kutoa wito kwa Wapalestina kila mahali kupigana.

Rais wa Palestina, Mahmoud Abbas alisema watu wake wana haki ya kujilinda dhidi ya ugaidi wa walowezi wa Israel.

Kulingana na shirika la habari la Reuters, Abbas alizungumzia kuhusu haja ya kutoa ulinzi kwa watu wake na kusisitiza kwamba ni haki ya watu wa Palestina ya kujilinda dhidi ya vikosi vya uvamizi.

Rais huyo alikuwa akiongoza mkutano wa dharura uliofanyika mjini Ramallah na maofisa wakuu wa Mamlaka ya Wapalestina.

**WATU 22 WUAWA**

Idara ya huduma za dharura za Israel ilisema kuwa takriban Waisraeli 22 wameuawa baada ya shambulizi la kushtukiza ambalo halijawahi kushuhudiwa kutoka kwa Wapalestina.

Wakati huo huo ,Wizara ya Afya ya Israel ilisema takriban watu 545 wamejeruhiwa katika mashambulizi ya Wapalestina.

**HAIJAWAHI KUTOKEA**

Kile kilichoshuhudiwa asubuhi ya jana imeelezwa hakina mfano katika kipindi cha zaidi ya miaka 15 tangu Hamas ilipochukua udhibiti wa Gaza.

Hatua hiyo inakuja baada ya miezi kadhaa ya ghasia na kuongezeka kwa mvutano kati ya Waisraeli na Wapalestina.

Hata hivyo, mapambano mengi yalikuwa yakitokea katika Ukingo wa Magharibi, ambao ni eneo ambalo Israel imelikalia tangu mwaka 1967, linalopakana na Jerusalem na Jordan.



Israel ilisema imeshambuliwa na kwamba Hamas imetangaza vita dhidi ya Israel.

Kulingana na maoni ya mhariri wa BBC kimataifa, Jeremy Bowen, alisema anadhani kuna uwezekano wa vikosi vya Israeli kuingia katika Gaza.

"Hali hii itaenda haraka na kuna uwezekano wa kuongezeka kwa mapigano. Swali moja kubwa ni nini kinachotokea sasa? Sio tu ndani na karibu na Gaza lakini kile kinachotokea katika Jerusalem na Ukingo wa Magharibi," alisema Bowen.

Alisema ni dhahiri kwamba hali tete iliyopo katika maeneo hayo itazidi kuwa mbaya kutokana na matukio ya sasa.

**KIFARU CHATEKWA**

Video moja iliyosambaa mitandaoni inaonyesha wapiganaji wa Palestina wakiruka kwenye kifaru cha Israel kilichotekwa na wanamgambo wa Hamas.

Picha hizo, ambazo shirika la habari la Reuters lilizipata, zinaonyesha wanamgambo wakiingia Gaza na gari la kijeshi kwa kile kinachosemekana walililiteka kutoka kwa wanajeshi wa Israel.

Msemaji wa Jeshi la Israel alikataa kusema chochote kwa waandishi wa habari kuhusu matukio hayo pamoja na Waisraeli kadhaa kukamatwa na wanamgambo wa Hamas.

Kundi la Jihad la Kiislamu ( Islamic Jihad) ambalo linaendesha harakati zake Gaza, linadai wapiganaji wake pia wamewakamata wanajeshi kadhaa wa Israeli.

Msemaji wake anayejiita Abu Hamza alisema kwenye chapisho la Telegram kuwa wanawashikilia wanajeshi hao.

"Tunathibitisha katika Brigedi za al-Quds kwamba sasa, shukrani kwa Mwenyezi Mungu, tunawashikilia askari wengi wa Israel ambao ni wafungwa mikononi mwetu." Alisema.

Islamic Jihad ni mojawapo ya makundi kadhaa ya wapiganaji wanaoendesha harakati zao huko Gaza.

Brigedi ya Quds ni tawi lake la kijeshi ambalo linashirikiana na Hamas.



# Simbachawene awapa rungu maofisa TAKUKURU rushwa miradi mikubwa

**Na Lusungu Helela,** MOSHI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene (pichani) amewataka wahitimu wa mafunzo ya awali ya maofisa uchunguzi na wachunguzi wasaidizi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwenda kuzuia na kupambana na rushwa kwenye miradi mikubwa ya maendeleo nchini ili kuokoa fedha zinazotolewa na Serikali.

Simbachawene alitoa wito huo jana mjini hapa wakati wa hafla ya kufunga mafunzo ya awali kwa maofisa hao 370 wa TAKUKURU yaliyofanyika katika Chuo cha Polisi (CCP).

Alisema serikali imedhamiria kuhakikisha maisha ya Watanzania yanakuwa bora zaidi kwa kutoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwamo ya elimu, afya na maji na si kuingia katika mifuko ya watu wachache.

Alisema malengo ya serikali ni kuhakikisha wahitimu hao wanakwenda kuzuia rushwa na ikishindikana wakapambane nayo kwani inapofusha macho na ni ukosefu wa ustaarabu katika jamii.

"Kazi yenu kuu sio kupambana na rushwa bali kuzuia kabla haijatokea na ndio maana Serikali imeamua kuajiri watumishi wa taaluma mbalimbali wakiwemo maofisa ununuzi, wahasibu, wasanifu majengo na wataalamu wa TEHAMA (Teknolojia na Habari na Mawasiliano) ili mkawe mbele kuzuia kulingana na taaluma zenu na kushauri ipasavyo mnapoona kuna dalili za rushwa," alisisitiza.

Simbachawene aliwataka wahitimu hao wa kutulia katika vituo vya kazi watavyopangiwa na kuachana na mawazo ya kuhamia sehemu nyingine kwa madai ya kutafuta masilahi zaidi.



"Wenye mawazo ya kuwa hapa TAKUKURU mnapita tu naomba niwaambie ukweli hakuna kitu kama hicho, ninyi mmepewa mafunzo maalum kwa manufaa ya kuwahudumia Watanzania kupitia TAKUKURU na sio kuhamia katika vituo vingine vya kazi," alisisitiza.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salum Hamduni alisema ajira hizo kwa wahitimu hao zilikuwa ni za kimkakati lengo ni kuhakikisha maeneo yaliyokuwa hayawezi kufikiwa na taasisi hiyo yanafikiwa kwa urahisi zaidi.

Alifafanua kuwa mafunzo hayo ambayo ni takwa la kisheria kwa kila mtumishi anayeajiriwa TAKUKURU, yamefanyika kwa miezi mitano kwa maofisa uchunguzi na mitatu kwa wachunguzi wasaidizi.

# Dirisha wanafunzi kwenda kusoma nje lafunguliwa

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Elimu Nje ya Nchi (GEL) umefungua dirisha kwa wanafunzi wanaotaka kwenda kusoma nje ya nchi muda wowote kwa muda wa mwaka mzima kuanzia sasa.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa GEL, Abdul Malik Mollel, wakati akizungumza wakati wa kuhitimisha wiki ya huduma kwa wateja iliyofanyika kwenye ofisi za wakala huyo.

"Kwa wanafunzi waliokosa masomo ya vyuo vya ndani ya nchi kuanzia sasa tumefungua dirisha la masomo kwa wanaotaka kwenda nje ya nchi," alisema na kuongeza:

"Watakwenda muda wowote hatutafunga kwa yeyote anayetaka kwenda aje tutamfanyia mchakato atakwenda."

Alisema mwanafunzi yeyote ambaye amekosa udahili kwenye vyuo vya ndani asifikiri amechelewa kwani vyuo vya nje vitaendelea kupokea wanafunzi muda wowote watakaohitaji kwenda uko kusoma.

Kadhalika, Mollel alisema GEL imejipanga kuongeza fursa za masomo kwa Watanzania wanaotaka kwenda nje ya nchi kusomea ubobezi kwenye Shahada za Uzamivu (PhD) na Shahada za Uzamili.

Alisema kwa sasa asilimia 90 ya wanafunzi wanaokwenda nje ya nchi kusoma kupitia GEL ni wa Shahada ya Awali na ngazi za vyeti na Astashahada, hivyo kuanzia sasa GEL itajitahidi kuongeza fursa za wanaotaka kusomea ngazi za juu za elimu.

Mbali na hivyo, alisema kutokana na mazingira mazuri ya elimu yaliyowekwa nchini, Tanzania itaanza kupata wimbi kubwa la wanafunzi kutoka nje kuja kusoma vyuo vya nchini.

Alisema ujio wa wanafunzi kutoka nje ya nchi si tu utasaidia kupata fedha za kigeni bali wanafunzi wa Kitanzania kupata marafiki ambao watawarahishia kupata ajira wanapomaliza elimu ya juu.

Alisema hatua ya wanafunzi kutoka nje ya nchi kuja kusoma Tanzania inaonyesha namna ambavyo mataifa mbalimbali duniani yamekuwa na imani na elimu ya juu inayotolewa nchini.

"Tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuifungua nchi na kusababisha iaminike dunia nzima kwa usalama na uwekezaji kwenye nyanja mbalimbali ikiwamo elimu na Rais Samia amekuwa akipita mataifa mbalimbali kutufungulia njia.

"Kwa miaka 16 ambayo Global Education Link imekuwepo hatukuwahi kufikiria hata siku moja kwamba Tanzania itapata wanafunzi wa kigeni, lakini tunaona kutoka mataifa mbalimbali wanakuja kila mwaka na wataendelea kuja na hii ni dalili njema kwamba Tanzania inazidi kuaminika," alisema Mollel

Aidha, alisema kwa miezi mitatu tu iliyopita Tanzania imepata wanafunzi wa kigeni zaidi ya 100 ambao watasaidia kuchangamsha uchumi kwa fedha za kigeni kwa muda watakaokaa nchini.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amewekeza kwa kiasi kikubwa kwenye sekta ya afya kwa hiyo GEL imeona ni muda mwafaka kuunga mkono juhudi za serikali kwa kuwatafutia fursa madaktari kwenda kusomea ubobezi kwenye fani zao.

Mollel alisema safari za nje ya nchi zinazofanywa na Rais Samia zimekuwa na manufaa makubwa nchini kutokana na idadi kubwa ya wageni wanaokuja kufanya shughuli mbalimbali nchini.

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Kitendawili nipe mji nikitegue nataka Mwanza nikale sangara



**Na Adam Fungamwango**

KUMEKUWA na mjadala kuwa wanamuziki na wasanii wa sasa hawaumizi kichwa kutunga nyimbo zao.

Ni hoja isiyopingika sana kwa kuwa asilimia kubwa wanakubali kuwa hakuna ubunifu mkubwa kwa sasa kwenye kutunga, kuimba na hata mapigo ya muziki.

Na hii inatokana na aina ya kizazi chenyewe cha sasa. Kizazi hakihitaji mambo mengi kutokana na mfumo wa maisha ya sasa yenye msongo wa mawazo kuanzia asubuhi mpaka mtu anapolala.

Kutokana na hilo, mwanamuziki na msanii haumizi kichwa kutunga wimbo, wala msikilizaji hahitaji hizo nyimbo zilizopangiliwa sana.

Ndiyo maana haishangazi kusikia wimbo ambao unataja jina la mtu kuanzia mwanzo hadi mwisho kama vile anamwamsha mwenzake usingizini, na mashabiki wanaupokea vyema na kuupenda. Ndivyo wanavyohitaji kwa sasa. Hawahitaji wimbo wenye maneno mengi, maudhui ya hekima na busara, au kufundisha, wao wanahitaji maneno machache na burudani na mapigo tu, basi!

Maisha yamekuwa na 'stresi' nyingi, kila kitu kinahitaji fedha, hawezi kuhangaika kupenda wimbo ambao una maneno ya mafumbo. Atakaa saa ngapi kufikiria hilo? Akiamka tu, gesi imeisha. Wakati anafikiria fedha ya kununulia gesi, umeme nao umezimika, unahitaji Luku. Kichwa kikianza kupata moto unagongewa hodi, watu anataka fedha za ulinzi. Wakati anabishana nao na kutaka wakupe muda, watu wa taka nao hao wametimba nyumbani.

Bado hujanunua vocha, bando na angalau umejitutumua kwanza umepata fedha ya kulipia umeme tu, familia inawasha televisheni unakuta kifurushi kimeisha.

Hapo unaweza kukuta zimebaki siku chake kabla ya kodi ya nyumba kwisha, akiba ya chakula nayo iko ukingoni.

Mtu wa aina hii utamwonea tu kumtungia wimbo wenye mashairi mengi yenye maonyo, badala yake anahitaji wimbo wa faraja tu, maneno machache laini na sebene lake tu.

Watunzi wa sasa nao wanaangukia kwenye kundi hilohilo. Nao pia ni binadamu wanakutana na changamoto hizo za maisha, hivyo wanashindwa kukaa na kutafakari kwa muda mrefu kupata nyimbo zilizopangiliwa vyema kwenye maudhui, mashairi na hata mapigo kama zile za zamani.

Lakini pia wameshafahamu walaji wao wa sasa hawataki vitu vigumu sana.

Zamani wanamuziki wengi walikuwa wanaajiriwa kama wafanyakazi wengine wa kampuni na mashirika mbalimbali ya serikali na binafsi.

Utakumbuka kuwa bendi nyingi za zamani zilikuwa za mashirika ya umma, hivyo wanamuziki waliifanya kazi ya muziki bila 'stresi' kwa sababu walikuwa na mishahara, posho, marupurupu kama wafanyakazi wa kawaida.

Pia kama nilivyosema huko nyuma hakukuwa na mambo mengi kama televisheni, jiko la gesi, vifurushi, simu za mkononi, hivyo hakukuwa na matumizi mengi ya fedha.

Ndiyo maana kulikuwa na nyimbo nyingi ambazo watunzi waliimba kwa lugha ya picha ili mashabiki na wapenzi wapate muda wa kutafakari, kubishana na kutegua ni kitu gani kilikuwa kikiimbwa.

Ndiyo maana hata kwenye taarabu kulikuwa na nyimbo kama 'Kijungu', 'Bunduki bila Risasi', 'Mgomba' na nyingine nyingi ambazo ziliimbwa kwa mafumbo na kila anayesikiliza alikuwa na tafsiri yake.

Muziki na dansi ulikuwa na nyimbo kama 'MV Mapenzi' namba moja na namba mbili za DDC Mlimani Park Orchestra, 'Chatu Mkali', na 'Kata ya Maji Ukweni' zilizopigwa na Orchestra Safari Sound, 'Ole Bado Wasumbuka' wa Juwata Jazz Band, 'Tausi' wa Urafiki Jazz Band na nyingi nyingi ambazo zilitungwa kwa mtindo wa lugha ya picha. Msikilizaji unatakiwa usikilize halafu utafakari nini kimezungumzwa.

Pamoja na yote, ukweli utabaki palepale kuwa wanamuziki wa zamani walifanya kazi kubwa, na hata hiki kizazi cha sasa licha ya changamoto zote bado wanazihitaji ili kuchangamsha ubongo wao.

Bendi ya MK Group ilitoa wimbo wa 'Kitendawili'. Ulitungwa mwanzoni mwa miaka ya 1990 na mwanamuzikI Paul Vitangi.

"Tegemea uliochokiona kwa macho, tegemeo ulikishika mkononi, tegemea ulichokimeza, usitegemee utakachotafuna.

Mwanangu nasikia ananivuta, lakini simoni ni kweli dunia ina maajabu yake, mwanangu natembea naye njiani bega kwa bega, lakini simshiki ni kweli dunia ina maajabu yake. Nilitembea nasikia mwanangu aniita, nikigeuka kumjibu haitiki jamani, walimwengu siyo wema mama yooo.

Kitendawili nipe mji nikitegue nataka Mwanza, nikale sangara, mwanangu ni mali niliyoitafuta kwa jasho, mali nimechuma naye mwenzangu kanigeuka, nguvu zangu zimepotea bure masikini, kweli walisema tenda wema nenda zako."

Pamoja na kufumba, lakini mtunzi mwishoni ametoa fumbo kwa kiasi fulani. Maana ya wimbo huu ni mwanamke mmoja aliyeishi na mwanamume wakiwa masikini, lakini baada ya kupata mali akatimuliwa.

Ndiyo maana mwanamke analalamika kuwa mali anazo alizochuma na mumewe, lakini kwa sasa hazimsaidii, ndiyo mtoto anayetembea naye njiani bega kwa bega, lakini akimwita haitiki.

Mwishoni anasema kabisa kuwa mali amechuma naye lakini mwenzake amemgeuka, akilalamika kupoteza nguvu zake wakati ule walipokuwa wakijenga nyumba, kuchuma mali, wakijinyima kwa kulala na njaa.

***Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James.

# Kafie kwenu-14

Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

FARIDA mwenyewe akatimuliwa na ujauzito wake, akarejea kwao Tabora kwenye kijiji cha Mtakwenda. Kwa bahati mbaya alimkuta shangazi yake ambaye alimlea baada ya kifo cha mama yake Tabu.

Alipojaribu kwenda kwa ndugu za baba yake mzee Katandukila hakupata msaada wowote kwa sababu walihofia akiishi pale anaweza kudai mali za baba yake mzazi, au kupata msaada kutoka kwa watu mbalimbali wenye huruma na wanaojua historia vizuri, hivyo kuwa hatari kwa ndugu waliodhulumu mali.

Alipoona hata kijijini kwenyewe hakueleweki akaamua kurejea Dar es Salaam.

Safari hii alifikia na kupewa hifadhi ya rafiki yake waliyetoroka naye kijijini walipokuja Dar.

Mwenzake baada ya kufanya kazi miaka miwili tu alipata mchumba, akamtoa kwenye kazi na kufunga naye ndoa.

Rozi alimhudumia rafiki yake waliyetoka naye kijiji kimoja kama ndugu yake akipata sapoti kutoka kwa mumewe.

Walikuwa na roho nzuri na mume wa Rozi alimpa huduma zote kama shemeji yake, hasa baada ya kupata historia yao kuwa wote hao wawili walitoroka kijijini Tabora na kukimbilia Dar es Salaam na kupata kazi za ndani kama mahausigeli.

Siku zake zikafika, Mungu akamjalia, akajifungua mtoto wa kiume na akamwita jina la babu yake, Katandukila.

Malezi ya awali hayakuwa na shida sana. Alipata kila kitu kutoka kwa Rozi na mumewe. Lakini Katandukila alipoacha kunyonya Farida akajiongeza. Akaona asingeweza kuishi kwa shoga yake milele wakati naye ana familia yake.

Akaamua kuondoka na kwenda kujitegemea. Rozi aliamua kumlipia kodi ya chumba kwa mwaka mzima maeneo ya Vingunguti.

Farida alingukia mikononi mwa mwanaume mmoja aliyeitwa Mbukusa. Huyu alikuwa mlevi kupundukia. Alisababisha Farida naye kuwa chapombe. Yeye na mumewe walikuwa wakienda wote kwenye vilabu vya pombe za kienyeji jioni na kurejea usiku.

Wakati mwingine njiani wanapigana na kutoana ngeu. Hayo ndiyo yalikuwa maisha ya Farida na bwana 'ake Mbukusa.

Hali hii ilimfanya Katandukila kusoma kwa tabu sana. Alimalizika kidato cha nne kwa tabu sana. Hakuweza kuendelea tena na masomo baada ya hapo.




**"Ulishawahi kuniuliza baba yako alipo na ni nani. Leo nataka nikwambie. Najuona kama siku zangu za kuishi zimefikia ukingoni, nitafanya dhambi kubwa kama sijakwambia asili yako.**

Baba yake mlezi alifariki kwa ugonjwa wa ini kutokana na kunywa pombe kali alizokuwa akichanganya na za kienyeji.

Mwaka mmoja na nusu baadaye Farida kaanza kuumwa.

Alipokwenda hospitali na kupimwa alionekana kuwa na ugonjwa wa figo. Moja ilikuwa haifanyi kazi na nyingine tayari ilishashambuliwa na ugonjwa unaotokana na kunywa pombe kupita kiasi.

Wakati bado nguvu hazijamuisha, alimwita kijana wake. Mtoto wake wa pekee, Katandukila.

"Mwanangu, mimi naona kama vile maisha yangu yamebaki mafupi tu duniani."

"Mama usiseme hivyo." Katandukila alimbembeleza mama yake.

"Siyo hivyo, naona kabisa kuwa sina maisha. Ndiyo maana nimekuita hapa kuna kitu nataka nikwambie ambacho kinaweza kukusaidia kwenye maisha yako."

Aliongea na sauti ya chini na upole kuashiria hana afya njema.

Katandukila, pamoja na kwamba hakupenda mama yake kuongea maneno kama yale lakini alitaka kusikia kitu gani atakachosema ambacho kitamsaidia kwenye maisha yake kwani wana maisha duni sana.

"Ulishawahi kuniuliza baba yako alipo na ni nani. Leo nataka nikwambie. Najuona kama siku zangu za kuishi zimefikia ukingoni, nitafanya dhambi kubwa kama sijakwambia asili yako.

Nitakufa kicho cha amani kama nitatekeleza hili. Baba yako ni mzee mmoja ambaye kwa sasa ni marehemu. Alikuwa anaitwa Joel Kamagi. Hakuwa mtu hohe hahe. Alikuwa ni tajiri, aliyemiliki mahoteli na viwanda. Siwezi kuorodhesha utajiri wake wote, lakini kweli ni tajiri.

Mwanangu, mimi nilipotoka kwetu Tabora katika kuhangaisha na dunia nilipata kazi za ndani kwake. Bahati mbaya sana mkewe alikuwa bize sana.

Na mimi kipindi hicho ni msichana mdogo, napendeza, akanitamani, nikapata ujauzito. Kwa sababu nilikuwa ninaishi japo, mkewe akatambua kama mimi mjamzito, akanitishia bastola ikabidi nimwambie ukweli wote. Nikafukuzwa pale na ujauzito, mpaka nikakuzaa wewe. Huyo ndiye baba yako, kwa sasa amefariki. Nilipata taarifa kuwa alifariki miaka minne iliyopita. Sikukwambia mapema ili usije ukasumbuka na kuumia na kumfuata kwa sababu ungeambulia kufukuzwa na kudhalilishwa, na kukataliwa pia, ungeumia sasa mwanangu.

Kama mimi nimefukuzwa, wewe mwanangu wasingeweza kukuelewa kabisa. Lakini nimeamua kumwambia ili ujue chimbuko na asili yako." alisema.

"Ahsante mama. Hilo nilitaka kulifahamu, nashukuru sana."

"Lingine ni kwamba nataka nikubatize mwanangu, nitakufa kwa amani kama nikiacha umebatizwa. Hukubatizwa utotoni, bado usichana ulikuwa unanisumbua."

Farida alilifanikisha hilo, Katandukila akabatizwa na jina lake la ubatizo likawa James.

"Mwanangu niko ukingoni kabisa mwa maisha yangu duniani. Mama yako nakufa nikiwa sijakuachia chochote cha kukufanya uishi vizuri duniani. Sijakuachia elimu wala mali zaidi ya matatizo. Hii yote ni kwa sababu ya historia ya maisha yangu na mikasa iliyonipata huko nyuma. Mwanangu James katika dunia hii hata kama ukiishi kimasikini sana. Hata kama watu wanatuchukia na kukudhalilisha. Usimchukie mtu yeyote, usilipe kisasi kwa yeyote atakayekufanyia ubaya. Machungu ya maisha yako duni yaweke rohoni siyo mdomoni.

Mpende na kumthamini kila mmoja, mkubwa na hata mdogo. Usimpende na kumyeyekea tajiri tu kwa sababu ya kutarajia kupata kitu kutoka kwake, fanya hivyo hata kwa watu duni, masikini na fukara kama wewe. Hawa huwa hawana pesa, lakini watakuombea baraka, dua na kukuongoza njia pia."

Ni usia wa mwisho wa Farida na kijana wake.

Wiki mbili tu baadaye alifariki dunia na kumuacha kijana wake akiishi kwenye chumba kimoja cha uani alichokuwa amepanga Vingunguti.

Kodi ilipoisha James alishindwa kulipia na kuamua kuondoka. Akarudi kulala kwa rafiki zake kama alivyokuwa akifanya hivyo wakati mama yake yupo hai.

Alipoanza kufanya kazi zake za vibarua, vingi alivipata akiwa Magomeni na Kinondoni. Ndipo alipoamua kupanga kwenye nyumba moja duni, Kinondoni Moscow.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# Izze Cheetah kuja kisasa zaidi kwenye mavazi

MBUNIFU wa mavazi anayekuja kwa kasi nchini, Izze Martin Cheetah, amesema anatarajia kutambulisha aina mpya ya nguo ambazo zitaleta mageuzi.

Akizungumza na BT jana, Cheetah, amesema tayari mitindo ya nguo zake imeanza kuonekana kwenye majukwaa mbalimbali ya maonyesho ya mavazi huku wasanii wakubwa wakipatwa na shauku ya kuvaa.

"Nikiwa kama Izze Martin Cheetah naona wazi tasnia ya mitindo itapaa kupitia brandi yangu ya Cheetah Fashion Creativity ambayo nimebuni mavazi ya kisasa zaidi na tofauti na yaliyozoeleka na wengi. Naomba Watanzania waendelee kuniunga mkono," amesema Cheetah.



# MARAFIKI MUSIC FESTIVAL 2023

## Singeli yawapagawisha mashabiki

WANAMUZIKI wa singeli nchini Dula Makabila na Baba Kash wamewapagawisha mashabiki wa muziki waliohudhuria Tamasha la Muziki la Marafiki katika viwanja vya Makumbusho jijini Dar es Salaam.

Tamasha hilo lilifanyika kwa muda wa siku tano na linahitimishwa leo mjini Bagamoyo, wasanii zaidi ya 150 kutoka mataifa mbalimbali walipanda jukwaani kutumbuiza.

Msanii wa Singeli Baba Kash ni miongoni mwa wanamuziki waliofanikiwa kuteka nyoyo za mashabiki na kufanya jukwaa kuwaka moto wa burudani.

Baba Kash alipanda jukwaani na kuimba nyimbo zake kama Panauma na kawaida na kusababisha mashabiki kutotulia vitini.

Akizungumza baada ya kutoa burudani Baba Kash amesema muziki wa singeli umeanza kupenya katika mataifa mengine na kupanda kwake jukwaani ni ishara ya kukubalika kimataifa.

"Nawashukuru waandaaji wa tamasha la Marafiki kwa kuona singeli ni sehemu ya muziki unaokubalika kimataifa, tumeanza kupenya na tukiongeza jitihada tutafika mbali," amesema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**HAALAND MKATABA MPYA**
KLABU ya Manchester City inafahamu mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland ana nia ya kuichezea Real Madrid, lakini wanataka kuanza mazungumzo kuhusu kuongeza mkataba wake, huku mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 ukiendelea hadi Juni 2027. (*ESPN*)

**MONK KUMRITHI PIRLO**

KOCHA wa zamani wa Swansea na Leeds United, Garry Monk ni jina linalohusishwa kuchukua nafasi ya Andrea Pirlo huko Sampdoria. (*SampNews24, via Sun*)

**OSIMHEN NA CHELSEA**

CHELSEA inasubiri kuona iwapo mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen atasaini mkataba mpya na Napoli, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 na mwakilishi wake bado wakiwa hawajafanya uamuzi wa kusalia katika klabu hiyo ya Italia au la. (*90 Min*)

**ALCARAZ ATAKIWA**

KLABU ya Brentford inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Southampton, Carlos Alcaraz mwenye umri wa miaka 20 wakati wa dirisha dogo la usajili Januari. ((*Standard*)

**MESSI KURUDI BARCA**

BARCELONA inafikiria kumrejesha mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 36 katika timu yake ya utotoni kwa mkopo Januari ikiwa Inter Miami itashindwa kufikia hatua ya mtoano ya MLS. (*Sport, via Mail*)

**CROUCH AKEJELIWA**

KLABU ya Burton Albion imechapisha chapisho la siri ikiukejeli uwezekano wa kurejea katika soka kwa mshambuliaji wa zamani wa Liverpool, Tottenham na England, Peter Crouch mwenye umri wa miaka 38. (*Mail*)

**BOATENG HANA TIMU**

MSHINDI wa Kombe la Dunia la Ujerumani, Jerome Boateng mwenye umri wa miaka 35 hana klabu baada ya kushindwa kupata mkataba na timu yake ya zamani Bayern Munich. (*Sun*)

**TOWNSEND YUKO LUTON**

WINGA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Crystal Palace na England, Andros Townsend mwenye umri wa miaka 32 yuko kwenye majaribio katika klabu ya Luton Town. (*Express*)

**MITCHELL KUBADILI URAIA**

MLINZI wa Crystal Palace, Tyrick Mitchell mwenye umri wa miaka 24 anaangalia uwezekano wa kubadili uraia kutoka England na kuuchukua wa Jamaica. (*Mail*)

**THOMPSON ALENGWA**
KLABU ya Bradford City inawalenga Steve Thompson na Neil Redfearn katika kutafuta kocha mpya kuchukua nafasi ya Mark Hughes. (*Star*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA YAMKUTA MAJANGA JUVENTUS

### Matokeo ya vipimo awamu ya pili yabaina kuwa...

**TURIN,** Italia

KWA mara nyingine tena Paul Pogba amekutwa na hatia ya matumizi ya dawa zilizopigwa marufuku michezoni baada ya matokeo ya vipimo vya awamu ya pili kubaini kuwa alitumia dawa za kusisimua misuli.

**Awali Septemba 11 mwaka huu Pogba alisimamishwa kwa muda na mahakama ya kitaifa ya kupambana na utumiaji wa dawa za kusisimua misuli ambapo aliomba ufanyike uchunguzi wa sampuli ya pili kwa ajili ya kuhakiki matokeo ya kipimo cha kwanza.**

Chini ya kanuni ya kuzuia matumizi ya dawa za kulevya, mfaransa huyo atawajibika kwa adhabu ya kifungo cha miaka minne, ambacho kinaweza kupunguzwa kwa nusu iwapo atathibitisha kwamba hakutumia dawa hizo kwa makusudi.

Mbali na taratibu za mfumo wa haki wa michezo wa Italia, uchunguzi wa kimahakama utafunguliwa na ofisi ya mwendesha mashtaka wa umma ya Turin, kwani dawa za kuongeza nguvu ni kosa la jinai nchini Italia.

Pogba ana siku saba za kuwasilisha utetezi wake kwenye mahakama ya kitaifa ya kupambana na dawa za kulevya, ambayo itachunguza kesi yake kabla ya kutekeleza adhabu hiyo utaratibu ambao unaweza kuchukua wiki kadhaa.

Kufuatia sakata hilo klabu ya Juventus imemsimamisha mshindi huyo wa kombe la Dunia mwaka 2018 kufanya mazoezi ya klabu hiyo huku ikisitisha malipo ya wastani wa mshahara wake wa euro milioni 8 kwa mwaka hadi 2026.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
ARSENAL
VERSUS
MANCHESTER CITY
1 | 2.83
X | 3.45
2 | 2.45

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA
MAOKOTO Deilee!
1. Razaki Salum - 0653 192 XXX
2. Richmondy Abdallah - 0654 753 XXX
3. Karim Chinyanga - 0656 374 XXX
4. Derick Makundi - 0657 222 XXX
5. Ramadhani Kelefu - 0672 234 XXX
6. Mseja Omary - 0673 534 XXX
7. Consolata Massawe - 0712 887 XXX
8. Fortunatus Komba - 0718 159 XXX
9. Tegnusi Mahingira - 0719 147 XXX
10. Said Abdallah - 0777 265 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP: DUNIA ILINIELEWA TOFAUTI



**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesisitiza kwamba wameweka kando sakata la VAR na kusisitiza watu walimuelewa vibaya alipozema mechi yao dhidi ya Tottenham Hotspur irudiwe.

Kocha huyo alisema anaamini kwamba mechi ilistahili kurudiwa baada ya makosa kutokea mwishoni mwa juma lililopita.

Klopp alisema: "Mimi ni mtu wa soka nadhani mechi inastahili kurudiwa. Mabadiliko hayakutokea kabisa. Muhimu kwa sababu kila mtu ametazama kwa jicho la tofauti tusisahau kuhusu hilo."

Ikaelezwa pia kuwa fowadi wa Liverpool Diogo Jota alilimwa kadi nyekundu kimakosa baada ya kuangaliwa upya.

Hata hivyo, Klopp akabadili kauli yake akidai watu walimuelewa vibaya alipozungumza hivyo kwani wachezaji wake wamesahau majanga yaliyotokea katika kipigo cha 2-1 walichopata dhidi ya Spurs.

"Vizuri sana, unataka Jota afanyaje kuhusu hilo? Najua itakuwa ngumu sana, nilipozungumza kuhusu mechi ya Spurs, imenithibitishia jinsi dunia ilivyo," Klopp aliongeza.

Baada ya kupokea kichapo cha kwanza katika Ligi Kuu England tangu msimu uliopita, Klopp alifanya mabadiliko ya wachezaji tisa ambao walicheza dhidi ya Union SG juzi Alhamisi kwenye mchezo wa kombe la Ligi ya Europa..

Kikosi cha Liverpool kilikuwa hatari na kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 yaliyowekwa kimiani na Ryan Gravenberch na Jota.

Kutokana na sakata la VAR mwishoni mwa juma lililopita, mabosi wa chama cha waamuzi walikiri kutokea kwa dosari kubwa baada ya Luiz Diaz kunyimwa bao halali dhidi ya Spurs.

Mabosi hao walithibitisha kuwa makosa ya kibinadamu yalichangia makosa kujitokeza katika mechi hiyo ya Ligi Kuu England, kwani afisa wa VAR alisahau kumwambia refa msaidizi abadili umamuzi wa refa wa kulikataa bao kwa sababu Diaz hakuwa ameotea.



# Bellingham atoa neno kufananishwa Zidane

**MADRID,** Hispania

BAADA ya kufanya mambo makubwa akiwa na uzi wa Real Madrid kwenye mashindano yote kwa muda mfupi, Jude Bellingham sasa anafananishwa na magwiji Zinedine Zidane na Di Stefano.

Bellingham mwenye umri wa miaka 20 raia wa England, amekuwa gumzo Ulaya na Hispania kwenye magazeti, TV, Redio na mitandao ya kijamii.

Mechi tisa, mabao nane na sasa wachambuzi wengi wanamuita Di Stefano mdogo, Zidane mdogo na ilikuwa hivyo kwenye vichwa viwili vya habari baada ya kufunga bao kwenye mchezo wa Ligi ya mabingwa Ulaya dhidi ya Napoli ya Italia.

Alipoulizwa kuhusu ulinganisho wake na nyota hao wa zamani wa Madrid, Bellingham alisema: "Ndoto yangu ilikuwa siku zote kuwa sehemu ya LaLiga katika kiwango kikubwa zaidi na naamini nitafika kwenye kiwango hicho."

Kocha wa Madrid, Carlo Ancelotti alisema: "Ninashangaa ana umri wa miaka 20 tu lakini anaonekana kama ana miaka 30 kwa sababu ya tabia na mtazamo wake.

"Sio kawaida kwa kijana wa miaka 20. Ana ubora mkubwa, nguvu za kimwili na ujuzi. Anan-ishangaza kama anavyofanya kwa kila mtu."

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# NI KIVUMBI LEO SIMBA, SINGIDA FG

**Na Saada Akida**

LIGI kuu Tanzania Bara inaendelea tena leo wakati wenyeji Singida Fountain Gate itakapowakaribisha simba kwenye Uwanja wa CCM Liti kuanzia saa 10 jioni.

Timu zote mbili zinahitaji alama tatu kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo huku Simba ikihitaji ushindi kwa ajili ya kurejea kilele ambapo kwa sasa wako nafasi ya pili wakiwa na alama 12 nyuma ya Azam FC wanaongoza kwa tofauti ya pointi moja baada ya ushindi wa juzi wa bao 1-0 dhidi ya Coastal Union.

Singida Fountain Gate FC ambao watakuwa nyumbani inahitaji alama tatu muhimu ili kujiondoka kwenda nafasi ya tisa katika msimamo wa ligi hiyo lakini pia wanahitaji ushindi ili kulipa kisasi kwa Wekundu hao wa Msimbazi waliowafunga msimu uliopita kwenye mchezo wa mzunguko wa pili wa ligi hiyo baada ya mzunguko wa kwanza kupata sare ya bao 1-1 wakiwa nyumbani.

Msimu uliopita Singida Fountain Gate FC walifanikiwa kupata sare ya bao 1-1 Novemba 9 mwaka janawakiwa kwenye uwanja wa Liti na mzunguko wa pili, February 3, 2023, Simba ilifanikiwa kushinda mabao 3-1 uwanja wa Benjamin Mkapa.

Simba iliendelea kuonyesha ubabe wao mbele ya Singida Fountain Gate baada ya kuwaondoa kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii kwa mikwaju ya penati 4-2 baada ya dakika 90 kutoka sare ya bao 1-1, uwanja wa Mkwakwani, Tanga.

Katika mchezo wa leo kwa mara ya kwanza utawashuhudia wachezaji wa zamani wa Simba, golikipa Beno Kakolanya na Michael Gadiel wakicheza dhidi ya waajiri wao hao wa zamani kwenye mchezo wa Ligi kuu baada ya kucheza nao kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii.

Singida Fountain Gate FC watashuka uwanjani leo wakiwa na kumbukumbu ya kushinda 1-0 mechi yao ya mwisho ya Ligi Kuu dhidi ya Mtibwa Sugar, Morogoro na Simba wakiifunga Tanzania Prisons mabao 3-1, Mbeya.

Kocha wa Simba, Roberto Oliviera kuelekea mchezo wa leo alisema malengo yake makubwa ni kushinda mchezo wa leo na wachezaji wake kufikia malengo wanayoyatarajia kwenye mchezo huo.

Alisema anaimani utakuwa mchezo mgumu kwa sababu ya ubora wa Singida Fountain Gate FC pamoja na kikosi hicho kuwa na wachezaji watatu kutoka, Simba akiwemo Kakolanya, Gadiel ambao wako kikosi cha kwanza na Joash Onyango ambaye atakosekana leo kutokana na kuwa majeruhi.

"Itakuwa mechi ngumu, wachezaji wao ni wazuri kuna wachezaji wametoka Simba, haitakuwa rahisi lakini tumejipanga vizuri kwa ajili ya kutafuta alama tatu muhimu," alisema Robertinho.

Naye kocha Msaidizi wa Singida Fountain Gate FC, Thambo Senong alisema wamefanya maandalizi mazuri na kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza mechi iliyopita na wako tayari kwa ajili ya kuwakabili Simba.

"Tunatambua ubora wa Simba tumejipanga vizuri, utakuwa mchezo wa kiufundi na mbinu kwa sababu tumejiandaa kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya," alisema Thambo.

**SOKA**



Vijana wakicheza mpira wa miguu katika viwanja vya kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam kama walivyokutwa na mpiga picha jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba, Yanga zakiri 'kazi ipo' CAF...

INATOKA UK. 24

"Tuna mikakati mizuri kuelekea mechi hizo, katika historia Simba iliwahi kucheza na timu zote, ikiwemo Wydad Casablanca ambayo hapa tulipata matokeo na kwenda kupoteza ugenini..

Kazi kubwa kwa sasa ni kuandaa timu ambayo itapata matokeo mazuri nyumbani na ugenini ili kutafuta pointi za kwenda hatua ya robo fainali ," alisema Robertinho.

Aidha alisisitiza kuwa kikosi chake kina wachezaji wenye viwango vizuri vinavyoweza kuwapa matokeo chanya timu hiyo na anaendelea kuiimarisha timu yake.

Simba imepangwa Kundi B, pamoja na timu za Wydad Casablanca ya Morocco, ASEC Mimosas ya Ivory Coast na Jwaneng Gallaxy ya Botswana.

Kwa upande wa Yanga, Rais wa Klabu hiyo Injinia Hersi Said alisema kundi walilopangiwa ni gumu kwa sababu lina bingwa mtetezi, Al Ahly, lakini kwa sasa ndiyo wakati wao kuionyesha dunia wana timu ya aina gani.

"Upande wetu tunamuona Al Ahly bingwa mtetezi, hivyo tutapata uzoefu kucheza na timu hiyo, ni kipimo kizuri kwetu kuona ni jinsi gani tumepiga hatua kama klabu ya mpira, naona kundi letu ni moja kati ya makundi magumu lakini sasa tunatakiwa tuweke jitihada ili tuwe moja kati ya timu mbili za juu zitakazokwenda hatua ya robo fainali," alisema Hersi kwa kifupi.

Yanga ipo Kundi D na timu za CR Belouizdad ya Algeria, Medeama na Ghana na Mabingwa Watetezi, Al Ahly ya Misri.

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 08/10/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1881 | Monza vs Salernitana | 1.71 | 3.86 | 4.84 |
| 13:30 | 2699 | Caykur Rizespor vs Samsunspor | 2.11 | 3.30 | 3.25 |
| 14:00 | 4416 | Marseille vs Le Havre | 1.52 | 4.44 | 5.99 |
| 14:30 | 3823 | Standard Liege vs Brugge | 4.39 | 3.94 | 1.66 |
| 15:00 | 3192 | Villarreal vs Las Palmas UD | 1.62 | 4.06 | 5.34 |
| 15:30 | 3651 | Ajax vs AZ Alkmaar | 2.21 | 3.61 | 2.77 |
| 15:30 | 4812 | Fortuna Sittard vs Twente | 3.47 | 3.77 | 1.86 |
| 16:00 | 2134 | West Ham vs Newcastle | 3.23 | 3.69 | 2.13 |
| 16:00 | 2153 | Brest vs Toulouse | 1.84 | 3.70 | 4.22 |
| 16:00 | 2529 | Lyon vs Lorient | 1.71 | 4.02 | 4.63 |
| 16:00 | 2584 | Frosinone vs Verona | 2.34 | 3.34 | 3.08 |
| 16:00 | 2723 | Besiktas vs Istanbulspor | 1.23 | 5.98 | 9.70 |
| 16:00 | 2816 | Wolverhampton vs Aston Villa | 3.39 | 3.50 | 2.13 |
| 16:00 | 3319 | Brighton vs Liverpool | 2.94 | 3.92 | 2.20 |
| 16:00 | 3972 | Lazio vs Atalanta | 2.72 | 3.33 | 2.62 |
| 16:00 | 4014 | Montpellier vs Clermont Foot | 1.82 | 3.86 | 4.12 |
| 16:00 | 5249 | Tanzania Prisons vs Mtibwa Sugar | 2.26 | 2.81 | 3.42 |
| 16:30 | 1808 | Dinamo Moscow vs Fakel | 1.49 | 3.96 | 5.97 |
| 16:30 | 4569 | Sekhukhune United vs Polokwane City | 2.46 | 2.67 | 3.23 |
| 16:30 | 4960 | Bayer Leverkusen vs FC Koln | 1.37 | 5.35 | 7.61 |
| 17:00 | 1293 | Aberdeen vs St Johnstone | 1.57 | 3.84 | 5.38 |
| 17:00 | 3376 | Brondby vs Viborg FF | 1.72 | 3.76 | 4.42 |
| 17:15 | 5401 | Atletico Madrid vs Real Sociedad | 1.91 | 3.46 | 4.23 |
| 17:30 | 2414 | BSC Young Boys vs FC Basel | 1.52 | 4.54 | 4.85 |
| 17:30 | 2965 | Lausanne vs Sport-FC Luzern | 2.47 | 3.46 | 2.56 |
| 17:30 | 4169 | Famalicao vs Vitoria Guimaraes | 2.54 | 3.14 | 2.69 |
| 17:30 | 4546 | Casa Pia Atletico vs CF Estrela | 2.00 | 3.19 | 3.69 |
| 17:45 | 1960 | Sparta Rotterdam vs PSV Eindhoven | 7.33 | 5.15 | 1.32 |
| 18:05 | 1218 | Lens vs Lille | 2.26 | 3.51 | 3.10 |
| 18:30 | 3459 | Arsenal vs Manchester City | 2.83 | 3.45 | 2.45 |
| 18:30 | 3718 | Bayern Munchen vs SC Freiburg | 1.18 | 7.80 | 13.35 |
| 19:00 | 1060 | Al Ahly Cairo vs Ismaily SC | 1.32 | 4.79 | 8.58 |
| 19:00 | 2865 | Pyramids vs Enppi Club | 1.46 | 3.99 | 6.78 |
| 19:00 | 3573 | Midtjylland vs Randers | 1.57 | 4.03 | 5.24 |
| 19:00 | 3686 | Spartak Moscow vs CSKA Moscow | 2.16 | 3.50 | 2.93 |
| 19:00 | 3726 | Hatayspor vs Konyaspor | 2.59 | 3.21 | 2.58 |
| 19:00 | 5294 | Cagliari vs Roma | 4.63 | 3.40 | 1.85 |
| 19:00 | 5514 | Kasimpasa vs Fenerbahce | 5.37 | 4.34 | 1.50 |
| 19:30 | 1012 | Alaves vs Betis | 2.77 | 3.12 | 2.71 |
| 19:30 | 3264 | Celta Vigo vs Getafe | 2.08 | 3.14 | 3.97 |
| 19:30 | 4072 | KAA Gent vs Racing Genk | 1.97 | 3.68 | 3.28 |
| 19:30 | 5027 | AEK Athens vs Panetolikos | 1.09 | 8.93 | 21.81 |
| 20:00 | 1604 | Hapoel Katamon vs Maccabi Tel Aviv | 5.24 | 3.63 | 1.55 |
| 20:00 | 4494 | Porto vs Portimonense | 1.13 | 7.33 | 15.85 |
| 20:30 | 1323 | Eintracht Frankfurt vs Heidenheim | 1.73 | 4.01 | 4.52 |
| 21:00 | 1239 | Aarhus vs Copenhagen | 3.06 | 3.26 | 2.27 |
| 21:45 | 1566 | Rennes vs Paris St Germain | 3.44 | 3.54 | 2.10 |
| 21:45 | 5396 | Napoli vs Fiorentina | 1.62 | 4.20 | 5.13 |
| 22:00 | 2879 | Granada vs Barcelona | 6.58 | 5.04 | 1.43 |
| 22:30 | 4407 | Sporting Lisbon vs FC Arouca | 1.24 | 5.57 | 9.94 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Oktoba 8, 2023

Nipashe




Pogba yamkuta majanga Juventus UK. 21




Mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize (kulia) akiwania mpira wa juu na mabeki wa Geita Gold FC wakati wa mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara jana kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza, Yanga walishinda goli 3-0. **PICHA: SALEHJEMBE**

## Simba, Yanga zakiri kazi ipo makundi CAF

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba na Yanga ambazo tayari zimewajua wapinzani wao kwenye hatua ya makundi zimekiri kuwa zipo katika makundi magumu, lakini zimeahidi kupambana kila mmoja ikitaka kuvuka hatua hiyo na kutinga robo fainali.

Aidha, muda mfupi baada ya kupangwa kwa droo hiyo juzi nchini Afrika Kusini, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, amezitaka klabu hizo kutohofia chochote, akizitia hamasa kuwa zinatakiwa kupambana bila kujali ukubwa wa timu zitakazocheza nazo, huku pia akizikumbusha pesa zilizoahidiwa na Rais Samia Suluhu Hassan Shilingi Milioni tano kwa kila goli litakalofungwa kuanzia kwenye hatua hii.

Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira, 'Robertinho' alisema kwa kutazama timu atakazokutana nazo kwenye hatua ya makundi licha ya kwamba ni nzuri na ngumu, lakini anaamini kikosi chake kitafanya vizuri.

Alisema kwa sasa Simba ni miongoni mwa timu kubwa Afrika hivyo hufurahia kucheza mechi ngumu kama hizi za Ligi ya Mabingwa Afrika hasa kwenye hatua hii.

INAENDELEA UK. 23

# Yanga yajitafuta, yajipata

### ●●● Baada ya kupoteza kwa Ihefu, yaishushia kipigo Geita Gold na....

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI watatu wa kimataifa, Muivory Coast, Pacome Zouzoua, Mburkina Faso, Stephane Aziz Ki, na Mkongomani Maxi Nzengeli, jana walituliza mioyo ya wanachama na mashabiki wa Yanga, kila mmoja alipofunga bao na kuipatia timu yao ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Geita Gold, kwenye mchezo wa ligi kuu Tanzania Bara uliochezwa uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Ushindi huo umekuja siku tatu tu baada ya kupoteza mchezo wa kwanza msimu huu walipokubali kipigo cha bao 2-1 kutoka kwa Ihefu FC.

Ushindi wa jana umewafanya Yanga kuwa nafasi ya pili ikiwa na pointi 12 nyuma ya vinara Azam FC wenye pointi 13 kwenye msimamo na juu ya watani wao Simba kwa tofauti ya magoli ingawa Simba wanaweza wakawazidi Yanga na Azam pointi leo kama wataibuka na ushindi kwenye mchezo wao dhidi ya Singida Fountain Gate.

Matokeo ya jana pia yanawabakisha Geita Gold katika nafasi ya 12 ikibaki na pointi zake nne, ikiwa imeshacheza mechi tano mpaka sasa.

Yanga ilianza mechi ya jana kwa kasi na kufanya mashambulizi ya nguvu mfululizo kwenye lango la Geita Gold kwa dakika sita. Shambulizi kali zaidi lilikuwa dakika ya tano pale Nzengeli alipoingia ndani ya eneo la hatari na kumtengea mpira Mudathir Yahaya aliyekuwa kwenye nafasi nzuri ya kufunga, lakini wakati akijiandaa, beki wa Geita Kelvin Yondani alifika na kuondoa mpira huo.

**Dakika mbili baadaye kipa wa Geita Gold FC, Sebusebu Samson aliiokoa timu yake kufungwa mapema , alipochumpa na kuda ka shuti lililopigwa na Pacome.**

Geita Gold ilifanya shambulizi la kwanza dakika ya nane ya mchezo, baada ya Elius Maguri kuwatoka mabeki wa Yanga Dickcon Job na Bakari Mwamnyeto, kabla ya kuachia shuti lililotoka nje kidogo ya lango.

Hilo lilikuwa shambulizi pekee la timu hiyo kipindi chote cha kwanza, huku kipa Djigui Diarra akiwa likizo kwa muda mrefu wa mchezo.

Maguri alilazimika kutolewa nje dakika ya 11 kwa kushindwa kuendelea na mchezo baada ya kugongana na beki wa Yanga Bakari Mwamnyeto, nafasi yake ikachukuliwa na Mashaka Valentino.

Kwa kipindi chote cha kwanza, Geita Gold ilionekana kupaki basi ikiwaacha Yanga wakitawala mpira kuanzia nyuma hadi katikati na kuwapa wakati mgumu mabeki wa timu mwenyeji.

Yanga ilianza kuhesabu mabao yake katika dakika ya 43 wakati Yao Kouassi alipoondoka na mpira kwenye wingi ya kulia hadi mwisho wa mstari, akawageuza mabeki wa Geita Gold FC na kumuwekea pasi safi Pacome akiwa nje kidogo ya eneo la hatari na kuachia shuti lililomshinda golikipa Sebusebu na kuipatia Yanga bao la kwanza.

Bao hilo linakuwa la tatu kwa Muivory Coast huyo msimu huu kwenye Ligi Kuu, akisajiliwa kwa mara ya kwanza kutoka Asec Mimosas.

Wakati wachezaji wa Geita Gold wakiwa wanajiuliza nini cha kufanya kusawazisha bao hilo sekunde chache kabla ya kupulizwa filimbi ya mapumziko, Stephane Aziz Ki aliipatia Yanga bao la pili baada ya kupiga shuti la kupasia nyavu akiwa ndani ya eneo la hatari kutokana na pasi safi ya Nzengeli.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko ya wachezaji lakini Yanga walionekana kunufaika zaidi na mabadiliko hayo ambapo katika dakika ya 68 walifanikiwa kupata bao la tatu lililofungwa na Nzengeli baada ya makosa ya kiungo Samuel Onditi ambaye alipewa mpira na Yondani nje kidogo ya eneo ya hatari, lakini alishindwa kuwa mwepesi kuuondoa na kujikuta akipokonywa na Mudadhir aliyempa pasi Nzengeli na kufunga kirahisi.

Baada ya bao hilo, wachezaji wa Geita Gold walionekana kama wameridhika kufungwa idadi hiyo ya mabao, na kuonekana kupasiana tu nyuma kwa kile kilichoonekana kupoteza muda na kupunguza uwezekano wa kufungwa idadi kubwa ya magoli.

Katika mchezo mwingine wa jana, Ihefu ambao walitoka kuifunga Yanga Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wao wa nyumbani wa Highlanders, Mbarali mkoani Mbeya, jana walikubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa KMC kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >